BARAZA LA WAWAKILISHI ZANZIBAR

# RIPOTI YA KAMATI YA KUDUMU YA UTALII BIASHARA NA KILIMO

YA

BARAZA LA WAWAKILISHI ZANZIBAR

KWA MWAKA WA FEDHA 2024/2025

FEBRUARI, 2025

YALIYOMO UKURASA

SEHEMU YA KWANZA ......................................................................................1

1.0 UTANGULIZI ...............................................................................................1

1.1 MUUNDO WA KAMATI ..............................................................................2

1.2 UTARATIBU WA KAZI ...............................................................................2

SEHEMU YA PILI .............................................................................................3

2.1 AFISI YA RAIS, KAZI, UCHUMI NA UWEKEZAJI .........................................4

2.2 MAPATO NA MATUMIZI ...........................................................................4

2.3 SEKTA YA UWEKEZAJI ..............................................................................7

2.4 UWEKEZAJI KWENYE VISIWA VIDOGO VIDOGO .......................................9

2.5 WAKALA WA UWEZESHAJI WANANCHI KIUCHUMI (ZEEA).......................12

2.6 IDARA YA USALAMA NA AFYA KAZINI.....................................................14

2.7 KITUO CHA MAFUNZO YA USARIFU WA MAZAO YA MBOGA
MBOGA NA MATUNDA ..............................................................................16

SEHEMU YA TATU ........................................................................................18

3.1 WIZARA YA UCHUMI WA BULUU NA UVUVI ..........................................18

3.2 MAPATO NA MATUMIZI .........................................................................18

3.3 SEKTA YA MAFUTA NA GESI ASILIA .......................................................21

3.4 UGAWAJI WA BOTI ZA UVUVI NA UKULIMA WA MWANI .........22

3.5 KILIMO CHA MWANI ..............................................................................24

3.6 UFUGAJI SAMAKI, MAJONGOO BAHARI NA KAA ...................................25

3.7 MRADI WA UJENZI WA MIUNDOMBINU YA USARIFU
WA DAGAA .................................................................................................27

3.8 MAMLAKA YA KUSIMAMIA UVUVI WA BAHARI KUU (DSFA)...................28

3.8 MAPATO NA MATUMIZI..............................................................29

SEHEMU YA NNE .......................................................................33

4.1 WIZARA YA UTALII NA MAMBO YA KALE ...........................................33

4. 2 UKUSANYAJI WA MAPATO .........................................................34

4.3 UTEKELEZAJI WA MIRADI YA WIZARA ..............................................38
4.4 KIVUTIO CHA UTALII CHA MTO FURAHA -PEMBA .............................40
4.5 MAMLAKA YA MJI MKONGWE ........................................................41
4.6 UKUSANYAJI WA MAPATO ............................................................41
4.7 UTEKELEZAJI WA MIRADI YA MAMLAKA YA MJI MKONGWE ...............42
4.8 MIRADI JUMUISHI INAYOSIMAMIWA NA MAMLAKA YA MJI

MKONGWE .................................................................................46

SEHEMU YA TANO ..........................................................................50
5.1 WIZARA YA BIASHARA NA MAENDELEO YA VIWANDA ......................50
5.2 WAKALA WA VIPIMO ZANZIBAR ..................................................52
5.3 TUME YA USHINDANI HALALI WA BIASHARA NA
KUMLINDA MTUMIAJI .................................................................53
5.4 TAASISI YA VIWANGO ZANZIBAR (ZBS) ..........................................56
5.5 KAMPUNI YA MWANI (ZASCO) ......................................................58
5.6 KIWANDA CHA KUKAMULIA MAFUTA YA MIMEA PAMOJA

NA SHAMBA LA MIKARATUSI TUMBE NA KISHINDENI.....................60

5.7 BARAZA LA UDHIBITI WA MFUMO WA UTOAJI WA LESENI ..............62

SEHEMU YA SITA
6.1 WIZARA YA KILIMO UMWAGILIAJI, MALIASILI NA MIFUGO ..............64
6.2 KITUO CHA UTAFITI WA KILIMO KIZIMBANI UNGUJA ....................66

6.3 CHINJIO LA KISAKASAKA UNGUJA ...............................................68

6.4 SHAMBA LA MALISHO YA WANYAMA ..........................................69

6.5 BONDE LA UMWAGILIAJI MAJI LA CHEJU B ..................................71

6.6 USIMAMIZI WA MASHAMBA YA KILIMO KWA MABIBI
NA MABWANA SHAMBA.........................................................72
6.7 KIWANDA CHA MINJINGU ARUSHA ............................................73
6.8 KIKUNDI CHA UFUGAJI WA NG'OMBE WA KISASA MPAPA..............74
6.9 HITIMISHO.........................................................................76

## RIPOTI YA KAMATI YA UTALII BIASHARA NA KILIMO YA BARAZA LA WAWAKILISHI ZANZIBAR

## KWA MWAKA WA FEDHA 2024/2025.

### SEHEMU YA KWANZA

### 1.0 UTANGULIZI

Kamati ya Utalii, Biashara na Kilimo ni miongoni mwa Kamati za Kudumu za Baraza la Wawakilishi iliyoundwa kwa mujibu Kanuni ya 119, Jadweli la Kwanza la Kanuni za Kudumu za Baraza la Wawakilishi, Toleo la mwaka 2024. Kamati hiyo imepangiwa kutekeleza majukumu Kama ifuatavyo:

i. Kufuatilia utekelezaji wa Sera na Mipango ya Wizara husika kwa kadiri Spika atakavyoelekeza kwa mujibu wa malengo yaliyowasilishwa katika Barazani wakati wa uwasilishaji wa Bajeti na hotuba nyengine za Waziri alizotoa katika Baraza;
ii. Kufuatilia utekelezaji wa miradi ya Maendeleo ya Kitaifa na miradi ya Wananchi ya Wizara husika;
iii. Kuchunguza na kufuatilia mapato na matumizi ya kila mwaka ya Serikali na kama matumizi yaliyofanywa yalizingatia thamani halisi ya fedha;
iv. Kuchambua mapendekezo ya Serikali kuhusu makadirio ya Wizara husika ya Mapato na Matumizi ya kila mwaka;
v. Kufuatilia utekelezaji wa maagizo ya Kamati yaliyotolewa kwenye ripoti ya Kamati ya mwaka uliotangulia;
vi. Kushughulikia Miswada ya Sheria itakayokabidhiwa kwake na Spika;
vii. Kuchambua ahadi zote za Wizara zilizo chini ya Kamati kama zitakavyokuwa zikitolewa katika Baraza na kufatilia utekelezaji wa ahadi hizo;
viii. Kufikiria jambo jengine lolote litakalopelekwa kwake na Spika;

Katika kutekeleza majukumu yaliyopo hapo juu, Kamati ya Utalii, Biashara na Kilimo inasimamia utekelezaji wa shughuli za Wizara tano zifuatazo:

- Afisi ya Rais, Kazi, Uchumi na Uwekezaji
- Wizara ya Uchumi wa Buluu na Uvuvi
- Wizara ya Biashara na Maendeleo ya Viwanda
- Wizara ya Kilimo, Umwagiliaji, Maliasili na Mifugo na
- Wizara ya Utalii na Mambo ya Kale.

### 1.1 MUUNDO WA KAMATI

Kamati ya Utalii, Biashara na Kilimo ya Baraza la Wawakilishi imeundwa na Wajumbe wanane wafuatao:

1. Mhe. Mtumwa Peya Yussuf - Mwenyekiti
2. Mhe. Hussein Ibrahim Makungu - M/Mwenyekiti
3. Mhe. Mwantatu Mbarak Khamis - Mjumbe
4. Mhe. Mihayo Juma Suleiman - Mjumbe
5. Mhe. Said Saleh Salim - Mjumbe
6. Mhe. Saada Ramadhan Mwendwa- Mjumbe
7. Mhe. Suleiman Makame Ali - Mjumbe
8. Mhe. Dr. Mohamed Ali Suleiman - Mjumbe

Aidha, Kamati ina makatibu watatu na msaidizi mmoja ambao ni:

1. Ndg. Yussuf Mkamba Mwinyi - Katibu
2. Ndg. Asma Ali Kassim - Katibu
3. Ndg. Abubakar Mahmoud Idd - Katibu
4. Ndg. Azmina Khamis Hamad - Msaidizi

### 1.2 UTARATIBU WA KAZI

Katika utekelezaji wa majukumu yake yaliyoainishwa na Jadweli la Kwanza la Kanuni ya 119 ya Baraza la Wawakilishi toleo la 2024, Kamati ilifanya kazi kwa utaratibu wa kupokea taarifa tofauti za kila robo mwaka (quarterly reports) za utekelezaji wa malengo ya Bajeti ya Wizara, kupokea taarifa za utekelezaji wa maagizo ya Kamati, kukutana na wadau mbali mbali wa sekta zinazosimamiwa na Kamati pamoja na kukagua baadhi ya maeneo na miradi mbali mbali inayosimamiwa na Wizara zinazohusika ili kuona hatua za utekelezaji zilizofikiwa, changamoto zilizopo na kutoa maoni, maagizo na ushauri wa kutatua changamoto hizo.

Kwa mwaka wa fedha 2024/2025, Kamati ilifanya kazi kwa mizunguko minne (4) kwa Unguja, Pemba na Tanzania Bara.

1. Mzunguko wa kwanza ulianzia tarehe 25 hadi tarehe 30 Machi 2024 kwa upande wa Unguja na kuanzia tarehe 02 hadi tarehe 06 April 2024 kwa upande wa Pemba.
2. Mzunguko wa pili ulianzia tarehe 12 hadi tarehe 16 Agosti 2024 kwa upande wa Pemba na kuanzia tarehe 19 hadi tarehe 23 Agosti 2024 kwa upande wa Unguja.
3. Mzunguko wa tatu ulianzia tarehe 04 hadi tarehe 08 Novemba 2024 kwa upande wa Unguja na kuanzia tarehe 10 Novemba hadi tarehe 15 Novemba 2024 kwa upande wa Tanzania Bara.
4. Mzunguko wa nne ulianzia tarehe 20 Januari hadi tarehe 24 Januari 2024, kwa upande wa Pemba na kuanzia tarehe 27 Januari hadi tarehe 31 Januari 2025 kwa upande wa Unguja

## SEHEMU YA PILI

## 2.1 AFISI YA RAIS, KAZI, UCHUMI NA UWEKEZAJI

Afisi ya Rais, Kazi, Uchumi na Uwekezaji ina jumla ya Wafanyakazi 454 inayojumuisha Wanawake 239 na Wanaume 215. Aidha, Ofisi imeundwa kwa Idara saba, Taasisi mbili zinazojitegemea pamoja na Bodi zake na Ofisi Kuu Pemba kama ifuatavyo:-
Idara hizo ni pamoja na: -

1. Kamisheni ya Kazi;
2. Ajira;
3. Usalama na Afya Kazini;
4. Maendeleo ya Vyama vya Ushirika;
5. Mashirikiano baina ya Sekta ya Umma na Sekta Binafsi;
6. Uendeshaji na Utumishi;
7. Mipango, Sera na Utafiti
8. Ofisi Kuu Pemba.

Taasisi zinazojitegemea: -

1. Mamlaka ya Kukuza Uwekezaji Zanzibar (ZIPA) na
2. Wakala wa Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi (ZEEA).

Bodi za Usimamizi za Taasisi :-

1. Bodi ya Wakurugenzi ya Mamlaka ya Kukuza Uwekezaji;
2. Bodi ya Wakurugenzi ya Wakala wa Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi;
3. Bodi ya Mishahara na
4. Bodi ya Ushauri wa Kazi.

## 2.2 MAPATO NA MATUMIZI

## FUNGU 006 (KAZI, UCHUMI NA UWEKEZAJI)

Kwa mwaka wa fedha 2024/2025 Afisi ya Rais, Kazi, Uchumi na Uwekezaji, kupitia fungu 006 (Kazi, Uchumi na Uwekezaji) ilitarajiwa kukusanya Mapato ya jumla ya shilingi bilioni tatu, milioni sabiini na nne, laki moja ishirini na tano, mia nane sitini na mbili nukta sita mbili (TSh. 3,074,125,862.62/=) hadi kufikia tarehe 31 Disemba 2024, Afisi imefanikiwa kukusanya mapato ya jumla ya shilingi bilioni mbili, milioni miatatu

thalathini na sita, laki sita thalathini na tatu elfu, miatatu thamanini na mbili (TSh. 2,336,633,382/=) sawa na asilimia 76% ya lengo kupitia vyanzo vyake vinne vya mapato, ikiwemo ada za Usajili na Ukaguzi wa Vyama vya Ushirika, Ada ya Ukaguzi wa Mikataba ya Ajira Nje ya Nchi, Ada ya Ukaguzi wa Maeneo ya Kazi na Vibali vya Kazi.

Kwa upande wa matumizi, Ofisi ya Rais, Kazi, Uchumi na Uwekezaji kupitia fungu 006 (Kazi, Uchumi na Uwekezaji) kwa kipindi cha Julai – Disemba, 2024-2025, ilikadiriwa kutumia jumla ya shilingi bilioni kumi na nne, milioni mia sita sitini na mbili, laki saba arubaini na moja elfu, na moja (TSh. 14,662,741,001/=) Kati ya fedha hizo, shilingi bilioni nne, milioni milioni miatatu arubaini na nne, na laki nne (TSh. 4,344,400,000/=) ni kwa ajili ya Mishahara; na shilingi bilioni kumi, milioni miatatu kumi na nane, na laki tatu arubaini na moja na moja (TSh. 10,318,341,001/=) ni kwa ajili ya Matumizi mengineyo. Wizara ilifanikiwa kuingiziwa na kutumia jumla ya Shilingi bilioni tano, milioni mia moja tisini na tano, elfu saba, mia sita sabini na nne ( TSh. 5,195,007,674/=) ambazo ni sawa na asilimia 35% ya makadirio.

## FUNGU 105 (WAKALA WA UWEZESHAJI WANANCHI KIUCHUMI)

Ofisi ya Rais, Kazi, Uchumi na Uwekezaji kwa Kipindi cha Julai – Disemba, 2024/2025 kupitia fungu 105 (Wakala wa Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi) lilikadiriwa kutumia jumla ya shilingi bilioni ishirini na tatu, milioni mia sita kumi na mbili, laki moja kumi na moja na mia tano (Tsh. 23,612,111,500.)

Kati ya fedha hizo, shilingi milioni mia sita ishirini na nane, laki nane na hamsini (Tsh. 628,850,000) ni kwa ajili ya Mishahara, na shilingi milioni ishirini na mbili, milioni mia tisa thamanini na tatu, laki mbili sitini na moja, na miatano.(Tsh. 22,983,261,500/= ) kwa ajili ya Matumizi mengineyo pamoja na Miradi ya Maendeleo.

Aidha, kwa upande wa matumizi halisi, Fungu 105 (Wakala wa Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi) iliingiziwa jumla ya shilingi bilioni moja, milioni mia tatu thalathini na tisa, laki sita sabiini elfu na mia sita sabiini (Tsh. 1,339,670,670). sawa na asilimia 5.7% ya makadirio. Kati ya hizo, jumla ya shilingi milioni mia nane ishirini na saba, laki tatu thamanini na tano, mia saba thalathini na tisa (Tsh. 827,385,739) zilitumika kwa ajili ya Mishahara ambayo ni sawa na asilimia 132 na shilingi milioni miatano kumi na mbili, laki mbili thamanini na nne elfu, mia tisa thalathini na moja Tsh. 512,284,931 zilitumika kwa

matumizi mengineyo ambazo ni sawa na asilimia 43 ya makadirio na hakuna fedha iliyotumika kwa ajili ya Miradi ya Maendeleo.

## 2.3 SEKTA YA UWEKEZAJI

Ni sekta ya kiuchumi ambayo inatoa fursa kwa wafanya biashara wa ndani na nje ya nchi kuendesha sehemu ya uchumi wa nchi kwa kutoa fedha zao kwa ajili ya kuanzisha shughuli fulani za kiuchumi na kugawana faida inayotokana na mitaji hiyo kwa mujibu wa makubaliano yaliyowekwa baina ya Serikali na muwekezaji.

Kwa kutambua umuhimu wa sekta hii kwa maendeleo ya nchi yetu, Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar imeunda chombo cha uratibu na usimamizi wa uwekezaji nchini ambacho ni Mamlaka ya Kukuza Uwekezaji Zanzibar iliyoundwa kwa Sheria ya Uwekezaji Zanzibar ya mwaka 2023. Aidha, Mamlaka hii inafanya kazi ya utekelezaji wa Sera ya Uwekezaji ya mwaka 2008 katika sekta zote zinazohusika. Hadi sasa, Zanzibar ina maeneo mbali mbali yaliyotengwa kwa ajili ya uwekezaji yakiwemo eneo la Fumba na Micheweni.

### MAENEO HURU YA UWEKEZAJI MICHEWENI

Dhamira kuu ya uimarishaji wa miundombinu ni kuyafungua maeneo hayo kwa kuboresha miundombinu kwenye maeneo ya uwekezaji na kufungua milango kwa wawekezaji kuweza kuyafikia maeneo hayo kwa urahisi.

Barabara zenye jumla ya 15.9km zimeweza kujengwa kwa awamu mbili tofauti kwenye eneo la Block A ambazo zimegharimu jumla ya shilingi bilioni ishirini milioni mia tisa sitini na tisa, laki tisa sabiini na nane, mia moja hamsini na tano (Tsh. 20,969,978,155.) Miundo mbinu ya umeme tayari imefika kwenye eneo la Block A. Miundombinu ya maji hadi sasa haijafika kwenye eneo hilo hata hivyo ZIPA inafikiria mpango wa kuwa na visima vyake kwenye eneo hilo ili kuweza kukidhi mahitaji.

Kwa upande wa Block B, hadi sasa hakuna uimarishwaji wowote uliofanyika isipokuwa ZIPA tayari imetangaza zabuni kwa ajili ya uimarishaji wa miundombinu ya Barabara zinazotegemewa kuwa na urefu wa 35km kwa kiwango cha lami.

Katika uimarishaji huu, jumla ya wananchi 217 waliathiriwa vipando vyao ambavyo malipo ya fidia yenye jumla ya shilingi bilioni moja, milioni mia moja tisini na sita, laki tisa arubaini na moja elfu (Tsh.1,196,941,000.00) zililipwa kwa awamu .

Hadi sasa ZIPA imeshatoa cheti cha uwekezaji kwa kampuni ya A&A International na kumpatia eneo lenye ukubwa wa 60 hekta kwa ajili ya uwekezaji wa

1. Chuo cha ufundi inayohusiana na mambo ya bahari kuu (Technical school)
2. Kituo cha kutotoa mazao ya bahari.
3. Chelezo (dry dog)
4. Bandari ya meli (port) ya kuegesha meli za uvuvi.
5. Kiwanda cha kuchakata mazao ya baharini (fish processing plant) na Cold room

Ili kuboresha hali ya uwekezaji kwenye maeneo hayo ZIPA ina mikakati ifuatayo;

1. Imeandaa bonanza "Micheweni marathon" linalotegemewa kufanyika mwezi wa April likiwa na lengo la kulitangaza eneo hilo kwa wawekezaji.
2. ZIPA imeandaa andiko la mradi "concept" ya kujenga warehouse 14 ambazo pamoja na huduma zinazoendana ili kurahisisha huduma kwa wawekezaji ambao watahitajia huduma hizo kama "storage facility" au kutumia kama viwanda vya uzalishaji, michoro na makisio ya andiko la Mradi "concept" hiyo imekamilika na ZIPA inategemea kuwasilisha Serikali kuu kwa lengo la kutafuta fedha za utekelezaji wa dhana hiyo.

## CHANGAMOTO

1. Kukosekana kwa miundombinu ya maji katika eneo hilo jambo linalopelekea kuzorota kwa shughuli za uwekezaji.
2. Hadi sasa eneo halijapata mwekezaji aliyesimama sawasawa na hivyo kuwafanya wananchi kutoelewa vyema dhana iliyokusudiwa.

## MAONI, USHAURI NA MAAGIZO YA KAMATI

**1.** Kutokana na hali ya eneo kubakia bila ya kuwekezwa kwa muda mrefu, Kamati inaomba Serikali kukamilisha mahitaji muhimu ya miundombinu, kuyatangaza kwa wawekezaji wa ndani na nje ili tupate tija iliyokusudiwa.

## 2.4 UWEKEZAJI KWENYE VISIWA VIDOGO VIDOGO

Mnamo mwaka 2018, Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar iliunda Kamati ya Wataalamu kwa lengo la kufanya tathmini ya Uwekezaji katika Visiwa vidogo vidogo na kuishauri Serikali juu ya hatua muafaka na bora za kuchukuliwa ili kuimarisha uwekeza katika visiwa hivi kwa lengo la kuleta matokeo makubwa yenye tija kwa Nchi na kwa jamii.

Zanzibar imezungukwa na visiwa vidogo vidogo ambavyo baadhi yake hutumika kwa makaazi, kuwa ni maeneo ya hifadhi na hata kwa shughuli za uwekezaji. Baadhi ya visiwa hivyo vilikodishwa kwa ajili ya uwekezaji. Ukodishaji wa visiwa vidogo vidogo unasimamiwa na Mamlaka ya Kukuza Uwekezaji Zanzibar (ZIPA).

Mamlaka ya Kukuza Uwekezaji Zanzibar ni Taasisi ya Serikali inayofanya kazi chini ya Sheria ya Uwekezaji Zanzibar ya mwaka 2023. Jukumu la msingi la Mamlaka hii ni kutekeleza sera na Sheria ya Uwekezaji kikamilifu kwa nia ya kuwavutia wawekezaji wenye tija kwa manufaa ya nchi na wananchi wake.

Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar ya awamu ya saba ilizuia ukodishaji wa visiwa hivyo baada ya kubaini kutokuwepo uratibu mzuri wenyemaslahi makubwa kwa nchi, hadi pale ilipoingia awamu ya nane na kuamua kulifanyia upembuzi wa kina suala hili kupitia kamati ya wataalamu. Baada ya Serikali kupokea Ripoti kutoka kwa Kamati ya Wataalamu iliridhia pendekezo la utoaji wa baadhi ya visiwa au maeneo ya baadhi ya visiwa kwa wawekezaji wenye tija kwa kuzingatia mazingira ya wananchi wanaoishi maeneo ya karibu, ili wananchi wanufaike na uwekezaji huo. Uamuzi huo una kwendasambamba na Dira ya Maendeleo ya 2050 ya Zanzibar inavyohamasisha Utalii wa Kiwango cha Juu na wenye tija na Mpango wa Maendeleo (2021-2026) unavyoelekezakujenga uchumi shindani, viwanda na maendeleo ya watu.

Mwaka 2021, Serikali kupitia ZIPA iliandaa tangazo la ukodishwaji wa visiwahivyo na ilitayarisha vipengele ikiwa kama ni muongozowa kufanya maombi ya uwekezaji katika visiwa hivyo. Hadi kufikia tarehe 30 Juni, 2024 jumla ya visiwa 16 vimekodishwa, ambavyo vitajengwa hoteli za kisasa zenye kuzingatia Uhifadhai wa Mazingira naRasilimali ya Bahari. Dola za Kimarekani Milioni ishirini na Sita (USD 26,000,000) zilikusanywa kama mahari (LAC) kupitia visiwa vilivyokodishwa na vinatarajiwa kuwekeza jumla ya Dola za Kimarekani milioni mia tatu themanini na nnenukta nne (USD 384.4 milioni). Visiwa vyote hivyovimekodishwa

kwa mujibu wa taratibu na Sheria ya Ardhi zinavyoelekeza ambapo kila mwekezaji amepatiwa miaka thelathini na tatu (33) na itaongezwa hadi kufikia tisini na tisa wakati muwekezaji atakapoomba kuongezewa.

## A) KISIWA CHA BAWE

Kisiwa hiki kipo Mkoa wa Mjini Magharibi ambacho amepatiwa mwekezaji anaejulikana kwa jina la Bawe Retreat Ltd. na jina la mradi ni Hotel ya Bawe Island by Cocoon collection. Mradi ulisajiliwa ZIPA mwezi Disemba 2021, ambapo mtaji utakaowekezwa ni Dola za Kimarekani milioni thelathini (USD 30,000,000). Wawekezaji walitakiwa kulipa kiwango maalum cha kupewa kisiwa hicho (mahari) yaani "Land Acquisition Cost" cha milioni mbili na nusu (USD 2,5 milioni) na imelipwa yote asilimia 100. Hata hivyo, mradi tayari umeshawekezwa mtaji wa dola za kimarekani milioni thelathini na nane (38,000,000) na ushafikia asilimia 90 ya utekelezaji wake. Mradi huu una majengo 129 yanayojumuisha vyumba vya kulala wageni, migahawa, spa, GYM, na mabwawa ya kuogelea.

Mradi huu una jumla ya villa 70. Jumla ya ajira zipatazo 400 zinatarajiwa kuzalishwa moja kwa moja kupitia mradi huu ambapo kila villa moja itahudumiwa na wafanyakazi wasiopungua 20.

Kwa kutambua umuhimu wa kutunza mazingira na ushirikishwaji wa wananchi katika miradi ya uwekezaji, mradi wa Bawe Island umewajengea wavuvi wa eneo hili madiko ya kisasa ili kuwapa fursa za kuendelea na shughuli zao za uvuvi na kuhakikisha kuwa mazingira ya maeneo hayo yanatunzwa na kulindwa. Pia mradi unasafisha maji ya bahari (disallination) kwa ajili ya matumizi ya kawaida ya hoteli ili kuepusha uchimbaji holela wa visima pamoja na kupitisha mabomba ya maji chini ya bahari ambayo yanachangia uharibifu wa viumbe hai vya baharini. Aidha, mradi huu unatumia nishati mbadala ili kuepusha uchafuzi wa mazingira, mradi unazalisha umeme wake wenyewe kwa kutumia vyanzo vinavyotokana na jua na upepo.

## B) KISIWA CHA PAMUNDA

Kwa kisiwa cha Pamunda, hivi ni visiwa viwili (Pamunda A &B) ambavyo vipo katika Mkoa wa Mjini Magharibi. Visiwa vyote viwili vimetolewa kwa mwekezaji aitwae P.S.VPamunda Limited. Mtaji wa makisio kwa kila kisiwa ni Dola

za Kimarekani miliomi 15 (USD 15,000,000). Kiwango maalumu cha kupewa kisiwa hicho yaani "Land Acqusition Cost" ni Dola za Kimarekani milioni tatu kwa kila kisiwa (USD 3,000,000) na mwekezaji amelipa asilimia 25 ya malipo hayo ambayo ni Dola za Kimarekani laki saba hamsini 750,000 kwa kila kisiwa. Tayari mwekezaji ameshakabidhiwa mkatabawa kukodishwa ardhi na kutayarisha Ripoti ya Athari za Kimazigira (EIA) na kupatiwa kibali cha ujenzi ambao unaendelea.

## CHANGAMOTO

1. Uendelezaji wa visiwa hivyo unagharimu kiasi kikubwa cha fedha kutokana na ugumu wa usafirishaji wa vifaa vinavyohitajika.
2. Kukosekana kwa misamaha ya kodi kwa uingizaji wa vifaa ambavyo wawekezaji wameomba

## MAONI, USHAURI NA MAAGIZO YA KAMATI

1. Ili kuongeza ajira kwa vijana wa Kizanzibari, Kamati inashauri kuwepo ushirikiano kati ya vyuo vya elimu ya juu na sekta zote rasmi nchini ili vyuo hivyo vifundishe fani zinazohitajika kwenye soko la ajira. Kadhalika, Wizara isimamiye vyema ajira ya sekta binafsi nchini kwani imebainika kuwa asilimia kubwa huajiri wafanyakazi kutoka nje ya Zanzibar jambo ambalo ni kinyume na sera na taratibu zetu.
2. Kamati inapendekeza marekebisho kwenye Sheria ya Uwekezaji ili kuingiza kipengele kitakachowataka wawekezaji wa kigeni kushirikiana na wazawa kwenye umiliki wa miradi ya uwekezaji nchini.
3. Kamati inaishauri Serikali kupitia Ofisi ya Rais, Fedha na Mipango kuweka utaratibu mzuri wa kutoa misamaha ya kodi kwa wawekezaji wa miradi ya kimkakati ili iweze kutekelezeka kwa ufanisi na kwa wakati uliopangwa.
4. Ili kuendeleza sekata hii ya Uwekezaji, Kamati inaiomba Serikali kupitia Wizara ya Nchi Afisi ya Rais Kazi Uchumi na Uwekezaji kusimamia kikamilifu vigezo vya miradi ya uwekezaji na kutowapa fursa wawekezaji wasio na sifa kuwekeza nchini.

## 2.5 WAKALA WA UWEZESHAJI WANANCHI KIUCHUMI (ZEEA)

Wakala wa Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi Zanzibar (Zanzibar Economic Empowerment Agency - ZEEA) imeanzishwa kwa Sheria namba 2 ya mwaka 2022 kwa lengo la kuimarisha mazingira wezeshi ya uwezeshaji wananchi kiuchumi ili kuongeza tija, uzalishaji, ufanisi na masoko ya bidhaa za wajasiriamali na wafanyabiashara nchini. Taasisi hii imeundwa kwa kuziunganisha Idara mbili zilizokuwepo awali; Idara ya Uratibu na Uendelezaji wa Programu za Wananchi Kiuchumi; na Mfuko wa Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi.

## MAJUKUMU YA (ZEEA)

Kwa mujibu wa kifungu namba 6 cha sheria namba 2 ya mwaka 2022, majukumu ya ZEEA ni:-

1. Kutoa ushauri kwa Serikali, Taasisi za umma na binafsi kwa mambo mahsusi na njia zinazolenga katika kushajihisha uwezeshaji kiuchumi Zanzibar;
2. Kuratibu programu za mafunzo na elimu, huduma za ushauri elekezi, masoko na utoaji wa mitaji kwa mjasiriamali au mfanyabiashara;
3. Kuwatambua, kuwahakiki na kuwaunganisha Wajasiriamali au Wafanyabiashara na Taasisi za Kifedha.
4. Kuanzisha na kuendeleza mfumo wa usimamizi wa taarifa wa shughuli za uwezeshaji wa wananchi kiuchumi katika sekta mbali mbali na na kuwezesha usambazaji wa taarifa;
5. Kupendekeza juu ya namna na njia za kuchukua zitakazohakikisha upatikanaji wa huduma za mikopo;
6. Kuchunguza au kukagua nyaraka zinazohusiana na mwenendo wa mjasiriamali au mfanyabiashara;
7. Kumtambua mjasiriamali au mfanyabiashara mwenye sifa kwa madhumuni ya kumuingiza katika programu za uwezeshaji;

8. Kutambua na kufanya utafiti wa masoko ya bidhaa na huduma zinazotolewa na mjasiriamali au mfanyabiashara;
9. Kuwezesha utoaji wa mkopo na kuhakikisha unarudishwa kwa wakati;
10. Kumuunganisha mjasiriamali au mfanyabiashara na vituo vya mafunzo vya amali n.k

**CHANGAMOTO**

1. Uhaba wa watendaji wa wakala.
2. Uchelewaji wa upatikanaji wa rasilimali fedha kwa mujibu wa 'Cash Flow' ambao unapelekea kuchelewa kwa utekelezaji wa baadhi ya kazi.
3. Kutokuwepo kwa Sheria na Kanuni za kuwabana wadaiwa sugu wa Mfuko wa Uwezeshaji.
4. Uchelewaji wa ulipwaji wa mikopo ambapo mikopo inayotolewa huchukuliwa kama ni ruzuku kwa wananchi.
5. Serikali za mitaa kutochangia kikamilifu asilimia kumi ya mapato yatokanayo na makusanyo ya ndani kama ilivyoelekezwa kwa mujibu wa Sheria.
6. Wananchi wengi kutokuwa na elimu ya uanzishaji wa miradi jambo linalopelekea kukosa fursa za mikopo ya uwezeshaji.

**MAONI, USHAURI NA MAAGIZO YA KAMATI**

1. Kamati inaishauri Serikali kuipatia Wakala wa Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi (ZEEA) kibali cha uajiri mara tu baada ya kukamilika taratibu za kiutumishi ili iweze kufanya kazi zake kwa weledi mkubwa.

2. Kamati inaiagiza Wizara kutoa mikopo midogo hadi mikubwa kwa makundi maalum yakiwemo watu wenye ulemavu ili kuwafanya wajikwamuwe kimaisha na kuweza kujitegemea.

3. Kamati inaishauri Serikali kuingiza fedha kwa wakati na kwa mujibu wa "Cash flow' Kwa lengo la kutekeleza ipasavyo shughuli za Wakala kwa wakati na kwa ufanisi mkubwa.

4. Kamati inaiagiza Wizara kuwasiliana na Wizara inayosimamia Mamlaka za Serikali za Mitaa kutekeleza wajibu wao kwa mujibu wa Sheria kwa kuchangia asilimia 10 ya mapato ya ndani kwenda katika Wakala wa uwezeshaji wananchi kiuchumi kwa lengo la kusaidia makundi maalum ya vijana, watu wenye walemavu na kina mama.

5. Kutokana na hali duni za vikundi vingi vilivokaguliwa na Kamati, tunaishauri Wizara kuweka utaratibu maalum wa kuwawezesha kufanya shughuli zao kwa ufanisi.

6. Wizara kwa kushirikiana na Wakala (ZEEA) iendelee kutoa elimu Zaidi juu ya uanzishaji wa miradi yenye tija kwa wananchi na inayoweza kupatiwa mikopo ili kila mwanachi aweze kunufaika kupitia mfuko huu wa uwezeshaji na hatimae marejesho ya mkopo yaweze kupatikana ipasavyo. Pia, Wizara ibuni mikakati itakayosaidia kupunguza kiwango cha mikopo chechefu.

## 2.6 IDARA YA USALAMA NA AFYA KAZINI

Usalama na Afya Kazini ni suala mtambuka ambalo linapaswa kuzingatiwa katika maeneo yote ya kazi kwa kuhakikisha kuwepo kwa nguvu kazi bora yenye afya, vifaa rafiki na wezeshi, pamoja na mazingira mazuri ya kufanyia kazi. Suala hilo linasimamiwa na Afisi ya Rais, Kazi, Uchumi na Uwekezaji kupitia Idara ya usalama na afya kazini (DOSH).

Idara hii ina jumla ya watendaji 13 (11 Unguja na 2 Pemba) ambao wamegawika katika Divisheni Nne zifuatazo:

1. Divisheni ya Afya
2. Divisheni ya usalama
3. Divisheni ya usajili na matukio
4. Divisheni ya mafunzo na uenezi

## CHANGAMOTO

1. Kuwepo kwa mapungufu kwenye sheria ya DOSH namba 8 ya mwaka 2005 ambayo imeonekana kutokidhi mahitaji ya kuikuza Taasisi na kuingiliana na sheria nyingine zilizopo.

2. Kuwepo kwa Kanuni moja tu inayoelekeza utekelezaji wa sheria ya DOSH namba 8 ya mwaka 2005.

3. DOSH kuendeshwa kama Idara chini ya kamisheni ya kazi jambo ambalo limepunguza ufanisi wake kiutendaji.

4. Upungufu mkubwa wa utaalamu na Wataalamu Idara DOSH.

5. Ufinyu wa bajeti na uingizwaji mdogo wa fedha zilizoidhinishwa kwa ajili ya matumizi ya DOSH.

6. Kukosa usimamizi katika Uchunguzi wa Afya za Wafanyakazi kutokana na ukosefu wa vifaa na upungufu wa wataalamu wa kuendesha shughuli hiyo.

7. Mafunzo na upimaji wa Afya kwa Wafanyakazi ni fursa ambayo haijatumika vyema katika kuboresha hali ya fedha.

8. Kutokuwepo kwa mfumo rasmi na matumizi madogo ya tehama katika utekelezaji wa shughuli za DOSH kunakopelekea kupungua wigo wa upatikanaji wa huduma pamoja utunzaji wa taarifa.

## MAONI, USHAURI NA MAAGIZO YA KAMATI

1. Kamati inaiomba Wizara kuandaa na kujenga hoja za kuunda OSH mpya yenye uthubutu kwa kufanya upembuzi yakinifu, upitiaji wa sheria kwa kuingizwa sura na vipengele vipya, kutengeneza Kanuni, miongozo na taratibu ili Taasisi hiyo iweze kujiendesha na kuchangia kwenye mapato ya Serikali.
2. Kamati inaitaka Idara ya Usalama na Afya Kazini kujitathmini na kupitia yote yaliyomo kwenye utendaji wao wa kazi na kufanya upembuzi yakinifu na kuwasilisha hoja za mapendekezo ya kuimarisha usalama na afya kazini kwa sekta ya umma na ya binafsi.
3. Ili kufanikisha utendaji wa majukumu DOSH kwa ufanisi, Kamati inaishauri Wizara kuitafutia vifaa, kuongeza watendaji wenye utaalamu, kuweka miundombinu na mifumo imara ya kisasa itakayowezesha utoaji wa huduma bora za kufikia sekta zote.
4. Kamati inaiomba Serikali kutoa elimu kwa watendaji wa Taasisi zote nchini ili waelewe taratibu za kufuata ili wapatiwe stahiki zao pindi wanapopata ajali kazini.
5. Kamati inaishauri Wizara Kuendeleza Mashirikiano baina ya Taasisi ya OSHA ya Tanzania Bara na DOSH ya Zanzibar utakaoweka msingi wa makubaliano ya ushirikiano unaolenga kukuza uwezo wa usimamizi wa sheria ya DOSH 2005 Zanzibar.
6. Wizara iimarishe matumizi ya tehama ili kuongeza uelewa pamoja na kusogeza huduma za DOSH karibu na wateja. Hii ni pamoja na kuanzisha DOSH website, Twitter, Facebook na social media platform nyingine ambazo zitawapa fursa wanajamii kuelewa huduma na umuhimu wa DOSH kwa maisha yao.

## 2.7 KITUO CHA MAFUNZO YA USARIFU WA MAZAO YA MBOGA MBOGA NA MATUNDA

Kituo cha Mafunzo ya Usarifu wa Mazao ya Mboga Mboga na Matunda kilichopo Kizimbani Unguja ni miongoni mwa Vituo vilivyokuwa vya Wakala wa Maendeleo ya Viwanda Vidogo Vidogo, Vidogo na vya Kati vinavyotumika katika kutoa mafunzo ya aina mbalimbali. Kituo hiki hapo awali kilijengwa na Wizara ya Kilimo, Umwagiliaji,

Maliasili na Mifugo kwa kushirikiana na Shirika la Kimataifa la Korea *"Korea International Cooperation Agency (**KOICA**)"* na kilitumika kama sehemu ya vituo vya mafunzo vya Chuo cha Kilimo kabla ya Chuo hicho kuunganishwa na SUZA.

Mnamo mwaka 2019, Wizara ya Kilimo na Maliasili ilikikabidhi rasmi kituo hicho kwa Wakala wa Maendeleo ya Viwanda Vidogo Vidogo, Vidogo na vya Kati (SMIDA) ili kiweze kutumika katika kutoa mafunzo na kuwaendeleza wajasiriamali wazalishaji wenye viwanda kwa lengo la usarifu aina mbali mbali za mazao ili waweze kuzalisha bidhaa zenye ubora kwa kuzingatia mifano bora ya uzalishaji wa viwandani.

Kituo kinatarajiwa kuwa na uwezo wa kuwahudumia wanafunzi/wajasiriamali 60 kwa wakati mmoja mara baada ya kukamilika matengenezo yake. Aidha, kitakuwa na mashine/vifaa vipya vya uzalishaji 35 pamoja na vifaa 25 tofauti vya maabara vyenye matumizi mbalimbali kwa ajili ya mafunzo ya vitendo kwa wajasiriamali, wazalishaji wenye viwanda vidogo vidogo, vidogo na vya kati Zanzibar.

**CHANGAMOTO**

1. Baadhi ya wajasiriamali waliopatiwa fedha za uzalishaji wa mboga mboga wanakabiliwa na uhaba wa taaluma kuhusiana na magonjwa yanayoibuka kwenye mazao yao.

**MAONI, USHAURI NA MAAGIZO YA KAMATI**

2. Kutokana na uhaba wa taaluma kwa magonjwa ya mazao ya mbogamboga yanayoibuka, Kamati inaiomba Wizara kuwapitia wajasiriamali hao mara kwa mara ili kuyabaini mapema na kwa kushirikiana na Wizara ya Kilimo itafute kinga na tiba ya maradhi husika.

## SEHEMU YA TATU

## 3.1 WIZARA YA UCHUMI WA BULUU NA UVUVI

## UTANGULIZI

Wizara ya Uchumi wa Buluu na Uvuvi imeundwa na Idara sita na taasisi nne zinazojitegemea kama ifuatavyo:

IDARA

1. Uendeshaji na Utumishi
2. Mipango, Sera na Utafiti
3. Uratibu wa Uchumi wa Buluu (Ukijumuisha Utafutaji na Uchimbaji wa Mafuta na Gesi)
4. Maendeleo ya Uvuvi na Mazao ya Baharini
5. Hifadhi za Baharini
6. Afisi ya Afisa Mdhamini – Pemba

TAASISI

1. Taasisi ya Utafiti wa Uvuvi na Mazao ya Bahari;
2. Kampuni ya Uvuvi;
3. Kampuni ya Maendeleo ya Utafutaji na Uchimbaji wa Mafuta (Zanzibar Petroleum Development Company);
4. Mamlaka ya Kudhibiti Utafutaji na Uchimbaji wa Mafuta (Zanzibar Petroleum Development Authority)

## 3.2 MAPATO NA MATUMIZI

Kwa Mwaka wa Fedha wa 2024/2025, Wizara imekadiriwa kukusanya mapato ya jumla ya Shilingi bilioni tano, milioni mia tisa ishirini na moja, na laki saba (Tsh. 5,921,700,000) kutoka vyanzo vyake vitano vya mapato Unguja na Pemba. Aidha, kwa kipindi cha Julai hadi Disemba, 2024 Wizara imekusanya jumla ya Shilingi bilioni mbili milioni mia tisa thamanini na nane, laki moja thalathini elfu mia tatu sitini na tano (Tsh. 2,988,130,365) kati ya Shilingi bilioni mbili, milioni mia tisa tisini na nane laki saba sitini na moja elfu, mia nne tisini na tisa (Tsh. 2,998,761,499) zilizokadiriwa, sawa na asilimia 99.7 ya makadirio.

Aidha, Wizara imeidhinishiwa kutumia jumla ya Shilingi bilioni sitini na sita,milioni mia moja ishirini na nane, laki moja sitini na sita elfu (Tsh. 66,128,166,000.) Kati ya fedha hizo Shilingi bilioni kumi milioni mia tisa thamanini na tano (Tsh.10,985,000,000) ni kwa Kazi za Kawaida na Shilingi bilioni hamsini na tano, milioni mia moja arubaini na tatu, laki moja sitini na sita elfu (Tsh. 55,143,166,000) ni kwa Kazi za Maendeleo. Kati ya fedha za kawaida, Shilingi bilioni nne, milioni mia moja thalathini, na laki mbili ( Tsh. 4,130,200,000) ni Mishahara, Shilingi bilioni mbili milioni mia tano na moja, na laki nne (Tsh. 2,501,400,000) ni kwa Matumizi ya Uendeshaji wa Ofisi na Shilingi bilioni nne milioni mia tatu hamsini na tatu na laki nne (Tsh. 4,353,400,000) ni Ruzuku kutoka SMZ. Kwa fedha za Ruzuku, Shilingi bilioni moja milioni mia moja sabini na saba na laki saba (Tsh.1,177,700,000) ni kwa ajili ya Taasisi ya Utafiti wa Uvuvi na Maliasili za Baharini Zanzibar, Shilingi bilioni mbili, milioni mia saba thamanini na nane, na laki tisa (Tsh 2,788,900,000 ni kwa ajili ya Mamlaka ya Utafutaji na Uchimbajiwa Mafuta na Gesi Asilia, na Shilingi milioni mia tatu thamanini na sita, na laki nane (Tsh. 386,800,000) ni kwaajili ya Kampuni ya Uvuvi Zanzibar (ZAFICO). Kwa upande wa Fedha za Miradi ya Maendeleo, Wizara imeidhinishiwa kutumia jumla ya Shilingi bilioni hamsini na tano milioni mia moja arubaini na tatu na laki moja na sitini na sita (Tsh 55,143,166,000) Kati ya fedha hizo, Shilingi bilioni thalathini na tisa (Tsh. 39,000,000,000 ) ni kutoka SMZ na Shilingi bilioni kumi na sita milioni mia moja na arubaini na tatu na laki moja sitini na sita (Tsh 16,143,166,000) kutoka kwa Washirika wa Maendeleo ambapo Shilingi bilioni kumi na tatu, milioni mia tatu arubaini na sita, na laki tisa tisini na nne (Tsh 13,346,994,000) ni mkopo na Shilingi bilioni mbili, milioni mia saba tisini na sita, laki moja sabini na mbili (Tsh 2,796,172,000) ni Ruzuku.

Kwa kipindi cha Julai hadi Disemba, 2024 Wizara imepatiwa jumla ya Shilingi bilioni kumi na sita milioni mia tano kumi na tano, na laki saba kumi na kumi na tano na mia tisa kumi na nane (Tsh.16,515,715,918) kati ya Shilingi bilioni thalathini na sita, milioni mia tisa arubaini na tisa, laki mbili na kumi na tatu, na mia nne sitini na moja (Tsh.

36,949,213,461) zilizopangwa sawa na asilimia 45 kwa Utekelezaji wa Kazi za Kawaida na Maendeleo. Kati ya fedha hizo Shilingi bilioni nne milioni mia moja ishirini na nane, na laki moja hamsini na tano na mia saba kumi na nane (Tsh. 4,128,155,718) kwa Kazi za Kawaida, ambapo Shilingi bilioni moja milioni mia saba sitini na saba laki tisa kumi na nne elfu, mia tano na saba (Tsh. 1,767,914,507) ni Mishahara, Shilingi milioni mia nne tisini na nane na elfu tisini na nane, mia tatu ishirini na saba (Tsh. 498,098,327) kwa Matumizi ya Uendeshaji wa Ofisi na Shilingi bilioni moja milioni mia nane sitini na mbili, laki moja arubaini na mbili na mia nane thamanini na nne (Tsh. 1,862,142,884) ni Ruzuku kutoka Serikalini kwa Taasisi ZAFIRI, ZAFICO na ZPRA. (Ambapo Shilingi milioni mia nne hamsini na saba laki sita arubaini na nane na mia nane kumi na tisa (Tsh. 457,648,819) ZAFIRI, Shilingi milioni mia moja tisini na saba na elfu saba, mia moja sabini na tano (Tsh. 197,007,175) ZAFICO na Shilingi bilioni moja milioni mia mbili na saba, laki nne thamanini na sita, na mia nane tisini (Tsh. 1,207,486,890) kwa ZPRA).

Kwa upande wa Utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo jumla ya Shilingi bilioni kumi na mbili, milioni mia tatu thamanini na saba, laki tano sitini, na mia mbili (Tsh. 12,387,560,200) zimepatikana, kati ya Shilingi bilioni thalathini na moja, milioni mia moja na saba, laki sita na ishirini na tano na mia mbili thalathini na mbili (Tsh. 31,107,625,232) zilizopangwa sawa na asilimia 40 ya makadirio Ambapo Shilingi bilioni kumi na moja milioni mia sita sabini na nne, laki mbili sabini na sita na mia nane na mbili (Tsh 11,674,276,802) kutoka SMZ na Shilingi milioni mia saba kumi na tatu laki mbili thamanini na tatu na mia tatu tisini na saba (Tsh. 713,283,397) kutoka Washirika wa Maendeleo.

### 3.3 SEKTA YA MAFUTA NA GESI ASILIA

Kwa mujibu wa Sheria ya Mafuta na Gesi Asilia Nambari 6 ya 2016, jukumu kuu la Mamlaka ya Udhibiti wa Utafutaji na Uchimbaji wa Mafuta na Gesi Asilia – Zanzibar

(ZPRA) ni Kudhibiti shughuli zote za Utafutaji na Uchimbaji wa Mafuta na Gesi Asilia Zanzibar pamoja na Kuhifadhi na kuendeleza data za Mafuta na Gesi Asilia Zanzibar.

Aidha, Kampuni ya Maendeleo ya Mafuta na Gesi Asilia Zanzibar (ZPDC) ni chombo maalum kilichoundwa kwa ajili ya kusimamia biashara ya mafuta na gesi asilia nchini.

## CHANGAMOTO

1. Kukosekana kwa wataalamu wa baadhi ya kada za Mafuta na Gesi Asilia hapa Zanzibar ikiwemo Jiofizikia (geophysics) na Jeokemia (Geochemistry) na Ukubwa wa gharama zinazohitajika katika kuwajengea uwezo wataalamu katika sekta ya mafuta na gesi asilia.

2. Uingizwaji mdogo wa fedha zilizoidhinishwa kwa ajili ya uendeshaji wa shughuli za mafuta na gesi asilia ambao umeipa wasiwasi Kamati yetu juu ya namna ya kuyafikia malengo yake ya kiutendaji.

3. Kukosekana kwa Kituo cha kudumu cha kuhifadhia Taarifa za mafuta na gesi asilia (NDR) ni jambo linalokwaza utekelezaji mzuri wa matakwa ya kifungu cha 81(4) cha Sheria ya Mafuta na Gesi Asilia Nambari 6 ya mwaka 2016.

## MAONI, USHAURI NA MAAGIZO YA KAMATI

1. Kamati inaiomba Serikali kutilia mkazo suala la ujenzi wa kituo cha kudumu cha uhifadhi wa taarifa za mafuta na gesi (NDR) ili tuepukane na changamoto inayotukabili ya kuhifadhi vipande vya Taarifa kwenye maeneo tofauti.

2. Kamati inashauri Serikali itafute (server) nyengine na kuiweka katika eneo jengine ili kuhifadhi vyema data zetu ambazo ni muhimu sana kwenye biashara hii ya mafuta na gesi duniani.

3. Kamati inaishauri Serikali kuongeza umakini katika kutafuta wawekezaji mahiri wa sekta ya mafuta na gesi ili kupata matunda ya rasilimali hiyo kwa maslahi ya wananchi kwa ujumla.

4. Kamati inaishauri Serikali, kupitia Wizara ya Uchumi wa Buluu na Uvuvi kuwa makini katika ugawaji wa vitalu vya mafuta baharini ili kujiepusha na migogoro isiyokuwa ya lazima.

5. Wizara iandae mpango maalum wa mafunzo ambao utalenga kuzijenga Taasisi zetu za mafuta na gesi kuwa na wataalamu wa kutosha ili kutekeleza majukumu hayo kwa ufanisi.

## 3.4 UGAWAJI WA BOTI ZA UVUVI NA UKULIMA WA MWANI

Serikali ya Mapinduzi Zanzibar inaendelea na mradi wa utengenezaji na ugawaji wa boti za uvuvi na mwani, ikiwa ni utekelezaji wa sera ya uimarishaji wa Uchumi wa Buluu nchini. Mradi huu ulitengeneza boti 1,027 za kisasa zenye vifaa muhimu ikiwemo mashine, vitafuta samaki (fish finders) na majokofu ya kuhifadhia samaki. Kati ya boti hizo, boti 500 za mita tano ni za mwani, boti 250 za mita 7 ni za uvuvi wa mishipi na boti 277 za mita 8 ni za uvuvi wa nyavu. Boti hizo na vifaa vyake vyote vilikuwa na gharama ya jumla ya shillingi Bilioni 22.8 kwa mgawanyo ufuatao:

| BOTI | PEMBA | UNGUJA | JUMLA |
|---|---|---|---|
| Mita 5 | 422 | 78 | 500 |
| Mita 7 | 103 | 147 | 250 |
| Mita 8 | 117 | 160 | 277 |
| **JUMLA** | **642** | **385** | **1,027** |

Kufuatia ugawaji huo wa boti 1,027 za uvuvi na ukulima wa mwani pamoja na zoezi la utoaji wa elimu ya uvuvi na ukulima wa mwani wa kisasa na endelevu pamoja na zana zake za uvuvi na za ukulima wa mwani zenye thamani ya shillingi bilioni ishirini na nne milioni mia sita kumi na nane na laki moja (Tsh. 24,618,100,000) Uzalishaji wa samaki umeongezeka kutoka Tani elfu thalathini na nane na mia moja na saba (38,107) zenye thamani ya shilingi Bilioni mia mbili na tano (Tsh. 205.35) kwa mwaka 2020 hadi kufikia Tani elfu thamanini na thamanini na tano (80,085) zenye thamani ya Shilingi Bilioni mia tano sitini na tisa nukta zero saba (Tsh. 569.07) kwa mwaka 2023 sawa na ongezeko la asilimia 110.2.

Uzalishaji wa zao la mwani umeongezeka kutoka Tani elfu nane na mia saba thamanini na tano (8,785) zenye thamani ya Shilingi Bilioni 5.387 kwa mwaka 2020 hadi kufikia Tani 16,653 zenye thamani ya Shilingi Bilioni kumi na sita nukta tano (16.5) kwa mwaka 2023 sawa na ongezeko la asilimia 89.6. Pia mradi huu umechangia katika kutoa ajira nyingi kwa vijana pamoja na kuchangia kukuza pato la Taifa.

## CHANGAMOTO

1. Kutoshirikishwa kikamilifu kwa Viongozi wa Serikali na Wawakilishi katika utoaji wa boti hizo hali inayopelekea Viongozi mbalimbali kutojua taarifa sahihi za utolewaji wa boti hizo kwa wananchi katika maeneo yao.
2. Urejeshwaji mdogo wa mikopo kwa waliopatiwa mikopo ya boti za aina mbalimbali za uvuvi. Kamati imeelezwa na uongozi wa CRDB kuwa viwango vya urejeshaji wa mikopo haviridhishi na hivyo hupelekea changamoto ya uhaba wa fedha kwa ajili ya ulipaji wa boti nyengine mpya ambazo zinatarajiwa kukopeshwa kwa wananchi wengine.

## MAONI, USHAURI NA MAAGIZO YA KAMATI

1. Kamati inaishauri Wizara inapotoa mikopo ni vyema kuwashirikisha Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi kutoka katika majimbo husika na viongozi wengine wa Serikali

ili kuwa na taarifa sahihi ya boti zilizotolewa kwa nia ya kurahisisha ufuatiliaji wa marejesho ya mikopo hiyo.

2. Kamati inaishauri Serikali kutoa elimu kwa wananchi juu ya urejeshaji wa mikopo kwa vile wapo baadhi ya wananchi baada ya kupatiwa mikopo hiyo wanakuwa wagumu kurejesha kwa kisingizo cha kuwa ni fedha ya Serikali na haistahili kurejeshwa na kupelekea kutopatikana mikopo hiyo kwa wananchi wengine ambao wana mahitaji ya mkopo huo.

## 3.5 KILIMO CHA MWANI

Mwani ni zao la biashara linaloajiri asilimia kubwa ya akina mama wa ukanda wa pwani wa Zanzibar. Ni zao la pili la biashara linalosafirishwa kwa wingi na ni sekta ya tatu kwa uchangiaji kwenye pato la Taifa. Kwa mujibu wa ripoti ya Shirika la Kilimo na Chakula duniani 2018, uzalishaji wa mwani hapa Zanzibar huweza kuchangia hadi Dola milioni 8 kwa mwaka ambao uzalishaji huo umeongoka.

Kamati ya Utalii, Biashara na Kilimo ya Baraza la wawakilishi inaipongeza Serikali ya Mapinduzi Zanzibar inayongozwa na Mheshimiwa Dr. Hussein Ali Mwinyi kwa juhudi zake za kuliiniua soko la mwani nchini kwa kuanzisha Kampuni ya mwani (ZASCO) ambayo imeanza kununua mwani kwa hatua ya awali na inatarajia kununua zaidi mara baada ya kuanza kazi kiwanda cha uchakataji mwani kilichopo Chamanangwe.

Kabla ya kuanzishwa kwa kampuni hii, wakulima wa mwani walikua wakinyonywa na mawakala wa kampuni binafsi, ambapo bei ya juu kabisa ya zao la mwani ilikua ni shilingi mia sita (600) lakini baada ya kuanzishwa kwa kampuni ya mwani (ZASCO) bei ya zao la mwani imepanda na kufikia shilingi elfu moja (1000) za kitanzania kwa mwani wa kawaida (spinosam). Hata hivyo, usimamizi mzuri unahitajika ili kuwafanya wazalishaji wa mwani kufaidi matunda ya kiwanda hicho.

## CHANGAMOTO

1. Mwani kukosa ubora kutokana na kuanikwa chini.

2. Kukosekana kwa mawakala wa kununua mwani siku hadi siku ili kukidhi mahitaji ya wananchi.
3. Upotevu wa vifaa vya ukulima wa mwani katika msimu wa Kusi.
4. Kuibuka kwa magonjwa ya mwani ambayo bado hayajulikani tiba yake.
5. Wakulima walio wengi ambao ni wanawake kutokua na vifaa vya kujiokolea na kushindwa kuogolea.

## MAONI, USHAURI NA MAAGIZO YA KAMATI

1. Kamati inashauri Wizara kuwawezesha wakulima wa mwani kwa kuwapatia nyenzo na utaalamu ili kuwapa fursa ya kuuza mwani huo kwa bei nzuri.
2. Kamati inaitaka Wizara kufanya Tafiti za magonjwa ya mwani ili kupata kinga na tiba za magonjwa hayo.
3. Taaluma zaidi inahitajika ili kuzalisha mwani bora ambao ndio wenye tija zaidi kwa wakulima.
4. Kamati inaishauri wizara kuvishajihisha vikundi vya wakulima wa mwani kwenda kujisajili rasmi ili vikundi hivyo viweze kukopesheka.
5. Wizara ya Uchumi wa Buluu na Uvuvi kwa kushirikiana na Wizara ya Biashara na Viwanda zibuni njia ya kuongeza uzalishaji na pia ziandae utaratibu bora wa ununuzi wa mwani ambao utawafanya wakulima kuuza mara kwa mara na kuepusha mlundikano wa mwani majumbani.

## 3.6 UFUGAJI SAMAKI, MAJONGOO BAHARI NA KAA

Ufugaji wa viumbe maji kama samaki, kaa na majongoo bahari ni shughuli ya kiuchumi kwa wanajamii wa visiwa vya Zanzibar. Wizara ya Uchumi wa Buluu na Uvuvi ina wajibu wa kuwasimamia, kuwaelimisha na kuwaendeleza wajasiriamali hao ili kuhakikisha wanazalisha kwa wingi na kiwango bora na hatimaye kupata soko la ndani na nje ya nchi.

Jumla ya mabwawa ya kufugia samaki ishirini (20) yamejengwa na kukabidhiwa vikundi kumi (10) kwa upande wa Unguja na vikundi kumi (10) upande wa Pemba. vizimba 60

vya ufugaji wa kaa vimejengwa Unguja (30) na Pemba (30) na mashamba ya kufugia majongoo bahari 100 yamejengwa Unguja (50) na Pemba (50).

Jumla ya mashamba 138 ya majongoo bahari, kaa, na samaki kati ya 180 Pemba yanaendelea vizuri sawa na asilimia 76.6. Aidha; Jumla ya mashamba ya majongoo bahari 30 kwa upande wa unguja yameharibika kati ya mashamba 50 yaliyojengwa na kugaiwa kwa wafugaji sawa na asilimia 60, na mashamba 12 ya (majongoo bahari 6 na kaa 6) yameonekana na changamoto kwa upande wa Pemba.

### CHANGAMOTO

1. Baadhi ya mashamba ya ufugaji wa viumbe maji yanakabiliwa na hitilafu za kiufundi tokea yalipokabidhiwa kwa Wizara mara baada ya kukamilika kwa ujenzi wake.
2. Kamati imebaini kuwa, baadhi ya mashamba yamekosa usimamizi imara kutoka kwa wajasiriamali waliokabidhiwa na kupelekea kutofikiwa lengo la kuanzishwa kwake.

### MAONI, USHAURI NA MAAGIZO YA KAMATI

1. Kutokana na hitilafu za kiufundi zilizojitokeza mapema kwenye mashamba ya ufugaji wa viumbe maji, Kamati inaagiza Wizara kuchukuwa hatua za haraka kurekebisha mashamba hayo ili yaweze kutumika kwa mujibu wa malengo yaliyokusudiwa. Aidha, Kamati inashauri Wizara kufuata kikamilifu taratibu za kupata wakandarasi wa ujenzi wa mashamba ya ufugaji wa viumbe maji ili kupata wajenzi bora watakaojenga mashamba imara kwa mustakbali mwema wa maendeleo ya uchumi wa Buluu na wananchi kwa ujumla.
2. Kamati inawaomba wajasiriamali waliokabidhiwa mashamba hayo kuyatumia ipasavyo kwani hiyo ni fursa ambayo wajasiriamali wengi wanaitaka.

## 3.7 MRADI WA UJENZI WA MIUNDOMBINU YA USARIFU WA DAGAA

Mradi wa ujenzi wa miundombinu ya usarifu wa dagaa umebuniwa na kuanzishwa katika mwaka wa fedha 2022/2023 ambapo utekelezaji wake ulipangwa kufanyika ndani ya

miaka mitatu. Mradi huu unatekelezwa katika maeneo mawili; Kama kwa upande wa Unguja na Ndagoni kwa upande wa Pemba.

Kwa Unguja, mradi huu unasimamiwa na Kampuni ya Uvuvi ZAFICO, ulikadiriwa kutumia jumla ya shilingi bilioni 23 kwa mujibu wa mpango mkuu "Master Plan". Gharama hizo ziliongezeka hadi kufikia jumla ya shilingi bilioni 38 baada ya serikali kuongeza mawanda "scope" ya mradi na kuagiza waanikaji wa dagaa kutoka Mangapawani na Fujoni wote waingie kwenye eneo la mradi wa Kama. Fedha hizo za mradi zinatokana na vyanzo vikuu viwili, Fedha za Maendeleo za Serikali ya Mapinduzi Zanzibar na mkopo kutoka benki ya CRDB.

Mkandarasi wa mradi huu ni JKU chini ya ushauri Elekezi wa Mamlaka ya kusimamia Majengo Zanzibar (ZBA).

Mradi unaotekelezwa eneo la Kama unaendelea na hatua zifuatazo: Ujenzi wa chanja za kuanikia Dagaa umefikia asilimia 80, Ujenzi wa Majengo ya kuchemshia Dagaa asilimia 85, Ujenzi wa Majengo ya kuoshea Dagaa asilimia 90, Ujenzi wa Majengo ya kupokelea dagaa asilimia 80, Ujenzi wa jengo la kuhifadhia kemikali asilimia 80 na Ununuzi wa majiko ya gesi asilimia 95.

Kwa upande wa Pemba, Mradi unatekelezwa katika eneo la Ndagoni katika bajeti ya Serikali ya miradi ya Maendeleo ya mwaka 2024/2025 baada ya fedha zake kupitia mradi wa uviko – 19 kupelekwa katika kiwanda cha Mwani mwaka 2022/2023 ambacho kilitakiwa kuanza sambamba na kiwanda cha Kama. Mradi huo ulianza mwezi wa Agosti, 2024 kwa Mkandarasi kuhamia eneo la ujenzi. Mradi unakadiriwa kutumia jumla ya Shilingi billion 7 hadi kukamilika kwake ambazo ni kutoka katika bajeti ya miradi ya maendeleo Afisi ya Rais Fedha na Mipango. Kamati ilikagua mradi huo na kujionea hatua zifuatazo: Ujenzi wa jengo la ghala umefikia asilimia 90, Ujenzi wa jengo la biashara asilimia 20, Interlocking pavment asilimia 20.

## CHANGAMOTO

1. Uchelewaji wa kuanza mradi kwa upande wa Pemba.

2. Kukosekana kwa miundombinu ya barabara ya kufikia eneo la mradi.

3. Mazingira duni ya kufanyia kazi kwa vibarua waliopo kwenye mradi.

4. Kukosekana kwa uzio kwenye andiko la awali la mradi.

## MAONI, USHAURI NA MAAGIZO YA KAMATI

1. Ili kukamilisha mradi huo kwa wakati, Kamati inashauri Mkandarasi kuongeza vitendea kazi hususan kwa eneo la Ndagoni.

2. Kamati inaishauri Wizara kuanza taratibu za uungaji wa umeme ili kukamilisha mradi huo kama ulivyopangwa.

3. Kutokana na umuhimu wa kulitunza na kulihifadhi eneo la mradi, Kamati inaitaka Wizara kujenga uzio katika maeneo yote ya mradi (Kama na Ndagoni) kwa ajili ya utunzaji wa maeneo hayo.

4. Kamati inaiagiza Wizara kumsimamia vizuri Mkandarasi ili kufuata masharti ya usalama na afya kazini kwa lengo la kulinda usalama wa watendaji wote wanaohusika kwenye mradi huo.

## 3.8 MAMLAKA YA KUSIMAMIA UVUVI WA BAHARI KUU (DSFA)

Mamlaka ya Kusimamia Uvuvi wa Bahari Kuu Tanzania imeundwa kwa Kifungu cha 6 cha Sheria ya Kusimamia na Kuendeleza Uvuvi wa Bahari Kuu Sura ya 388 ya mwaka 2020 ili kutekeleza majukumu yafuatayo:-

- Kusimamia na kudhibiti uvuvi na shughuli zinazohusiana na uvuvi katika Ukanda Maalum wa Uchumi wa Bahari kwa mujibu wa sheria na kanuni za uvuvi wa bahari kuu;

- Kuainisha na kuweka ada na tozo mbalimbali zinazotokana na shughuli za uvuvi wa bahari kuu ikiwemo utoaji wa leseni, ruhusa na vibali vya uvuvi;

- Kuainisha na kuendeleza njia zozote muhimu zitakazowezesha kuzalisha kipato na manufaa ya kijamii;
- Kuandaa na kuratibu programu za kisayansi, kiuchumi, kijamii na tafiti nyingine zinazohusiana na uvuvi katika bahari kuu;
- Kujadiliana na kuingia mkataba wowote, makubaliano au mashirikiano na taifa au taasisi nyingine inayohusiana na jambo lolote ndani ya maudhui ya sheria inayohusiana uvuvi wa bahari kuu;
- Kulinda mazingira ya bahari ya Ukanda Maalum wa Uchumi Bahari; na
- Kufanya na kutekeleza jambo jingine lolote au kitu kinachotakiwa au kuruhusiwa kufanywa kwa ajili ya kufikia malengo, maudhui na sheria inayohusiana na uvuvi wa bahari kuu.

## 3.8 MAPATO NA MATUMIZI

Mamlaka (DSFA) imefanikiwa kukusanya jumla ya Shilingi bilioni tatu, milioni mia tisa na saba, laki saba na thamanini (Tsh. 3,907,780,000) katika kipindi cha Julai – Disemba 2024 kwa kuuza leseni 27, vibali viwili (2) vya kuvua nje ya mipaka ya Tanzania (ATF), na vibali vitano (5) vya uwakala wa meli.

Aidha, katika utekelezaji wa majukumu yake kwa mwaka 2024/2025, Mamlaka (DSFA) imeidhinishiwa matumizi jumla ya shilingi bilioni nne, milioni mia mbili thalathini na saba, laki moja tisini na tano, mia tano na tisini na mbili (Tsh. 4,237,195,592) kwa ajili ya kutekeleza kazi mbalimbali ambapo fedha zote zinatokana na vyanzo vya ndani.

Hadi kufikia tarehe 31 Desemba, 2024, Mamlaka (DSFA) imetumia jumla ya Shilingi bilioni tatu, milioni mia moja sabini na sita, laki mbili na kumi na nne na mia tisa sitini na tatu (Tsh. 3,176,214,963) sawa na asilimia 75% ya makadirio ya kipindi hicho.

## UKAGUZI WA MELI ZINAZOOMBA LESENI ZA UVUVI WA BAHARI KUU NA ZINAZOFUNGA GATI NCHINI

Kwa kipindi cha Julai- Disemba, 2024 jumla ya Meli 12 zilizoomba leseni na vibali zilikaguliwa ambapo meli mbili (2) zilikaguliwa nchini na meli tisa (9) zilikaguliwa katika bandari ya Victoria, Ushelisheli; na meli moja (1) ya kigeni iliyofunga gati katika Bandari ya Dar es Salaam.

## MAJUKUMU MENGINE YA MAMLAKA (DSFA)

Mamlaka (DSFA) kwa kipindi cha Juali - Disemba, 2024 imefanikiwa kutekeleza shughuli zifuatazo:

- Kufanya mapitio ya Sheria ya Usimamizi na Uendelezaji wa Uvuvi wa Bahari Kuu, Sura 388 ya mwaka 2020 kwa kushirikiana na Wizara ya Mifugo na Uvuvi, Wizara ya Uchumi wa Buluu na Uvuvi, Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali (SMT/SMZ).
- Kufanya Ufuatiliaji wa mienendo ya meli za uvuvi kwa kutumia mifumo ( VMS na AIS) na kutoa taarifa kwa Mkurugenzi Mkuu. Aidha, kazi hii inatekelezwa kwa mashirikiano ya karibu na KMKM, jeshi la wanamaji (Navy), Polisi Wanamaji, Wizara ya Uchumi wa Buluu na Uvuvi na Wizara ya Mifugo na Uvuvi.
- Kutoa Elimu Kuhusu Uvuvi wa Bahari Kuu na mfumo wa ufuatiliaji wa mienendo ya Vyombo vya Uvuvi (VMS) kwa makamanda wa Navy Kigamboni, Disemba 2024.
- Kutoa mafunzo na kujenga uwezo wa mabaharia 14 nchini kuhusu Ukaguzi na Uvuvi wa Bahari Kuu
- Kufanya ukaguzi wa Shehena ya samaki wasiolengwa (by-catch) kiasi cha tani 80.88 kilichopokelewa mwezi Novemba 2024 kupitia Bandari ya Dar es Salaam.
- Kutoa mafunzo ya Uvuvi kwa Wavuvi wadogo ili waweze kuvua katika Bahari Kuu na Uvuvi Endelevu

## CHANGAMOTO

1. Uwekezaji mdogo katika uvuvi wa bahari kuu nchini
2. Kukosekana kwa Miundombinu muhimu kuhudumia meli za uvuvi wa bahari kuu

3. Matumizi ya fedha nyingi kutumika katika Usimamizi na ulinzi wa rasilimali za uvuvi wa bahari kuu

4. Upatikanaji wa takwimu sahihi za uvuvi

5. Wazawa kutoshiriki katika uvuvi wa bahari kuu

**MAONI, USHAURI NA MAAGIZO YA KAMATI**

1. Kamati inaiomba Serikali kukamilisha mchakato wa ujenzi wa bandari mahsusi ya uvuvi itakayokuwa na uwezo wa kuhudumia meli zenye kufanya uvuvi wa bahari kuu nchini.

2. Ili kuongeza uwekezaji wa bahari kuu nchini, Kamati inashauri Serikali kupitia Mamlaka (DSFA) kuingia makubaliano na makampuni ya uvuvi ya nje na ndani ili kuwekeza katika sekta hiyo nchini. Aidha, Kamati inaishauri Mamlaka (DSFA) kushirikiana na vituo vya uwekezaji nchini (TIC na ZIPA) katika kutangaza fursa za uwekezaji katika uvuvi wa bahari kuu na kuweka mazingira bora zaidi ya uwekezaji katika uvuvi wa bahari kuu.

3. Kwa ajili ya kuhakikisha upatikanaji wa takwimu sahihi za uvuvi, Kamati inashauri Mamlaka (DSFA) Kupitia upya Agenda ya Utafiti katika Ukanda wa Uchumi wa Bahari (EEZ) 2020-2025 na kufadhili tafiti za uvuvi wa bahari kuu nchini.

4. Kamati inaunga mkono matumizi ya teknolojia (drone) katika usimamizi wa rasilimali za uvuvi wa bahari kuu.

5. Kamati imebaini kuwa ushiriki mdogo wa wazawa kwenye uvuvi wa bahari kuu unatokana na uhaba wa taaluma na nyenzo. Hivyo, tunaiomba Serikali kuwajengea uwezo wavuvi wetu ili waweze kuingia bahari kuu na kufaidika na uvuvi huo mkubwa kwa faida yao na Taifa kwa ujumla.

## SEHEMU YA NNE

## 4.1 WIZARA YA UTALII NA MAMBO YA KALE

Wizara ya Utalii na Mambo ya Kale ina dhamana ya kusimamia Sekta Kuu mbili ambazo ni Sekta ya Utalii na Sekta ya Mambo ya Kale. Sekta hizi hujumuisha Kamisheni moja, Idara nne, Mamlaka moja na Ofisi Kuu Pemba ambazo ni: -

1. Kamisheni ya Utalii Zanzibar

2. Idara ya Utalii
3. Idara ya Makumbusho na Mambo ya Kale
4. Mamlaka ya Hifadhi na Uendelezaji Mji Mkongwe
5. Idara ya Uendeshaji na Utumishi
6. Idara ya Mipango, Serana Utafitina
7. Ofisi Kuu Pemba

## PROGRAMU KUU ZA WIZARA YA UTALII NA MAMBO YA KALE

Wizara ya Utalii na Mambo ya Kale inatekeleza Malengo na Majukumu kwa kufuata Mfumo Maalumu wa Bajeti (Program Based Budget, PBB), ambapo Wizara inasimamia programu kuu tano na programu ndogo tatu.

**Programu Kuu za Wizara ni : -**

I. Programu ya Maendeleo ya Makumbusho, Mambo ya Kale na Uhifadhi wa Mji Mkongwe.

II. Programu ya kusimamia Maendeleo ya Utalii.

III. Programu ya Utangazaji na Uhamasishaji Utalii.

IV. Programu ya Uendelezaji na Uratibu wa Utalii

V. Programu ya Utawala na Uendeshaji katika Sekta ya Utalii na Mambo ya Kale.

**VI. Programu Ndogo za Wizara ni : -**

i. Kuratibu na kusimamia Mipango Mikuu ya Wizara.

ii. Utawala na Uendeshaji katika Sekta za Utalii na Mambo ya Kale.

iii. Kuratibu na Kusimamia Utawala, Uendeshaji na Mipango ya Ofisi Kuu Pemba.

## 4. 2 UKUSANYAJI WA MAPATO

Wizara ya Utalii na Mambo ya Kale kwa kipindi cha robo mbili Julai – Disemba mwaka wa Fedha 2024/2025 Wizara ilipanga kukusanya jumla ya shilingi bilioni mbili, milioni mia nane thalathini na tano, laki nane sabini na mbili (Tsh 2,835,872,000/=) na kufanikiwa kupatiwa jumla ya shilingi bilioni nne milioni mia saba kumi na mbili na laki tisa thalathini, na mia mbili sitini na saba (Tsh 4,712,930,267/= ) sawa na asilimia 166.

## MATUMIZI YA WIZARA

Kwa upande wa matumizi mengineyo kwa kipindi cha robo mbili, Julai – Disemba kwa mwaka wa fedha 2024/2025 Wizara imekadiria kutumia jumla ya shilingi bilioni moja milioni mia saba kumi na tatu na elfu kumi na moja na mia nne (Tsh. 1,713,011,400) na kufanikiwa kutumia jumla ya shilingi milioni mia saba tisini na tatu na laki tano hamsini na tatu na sitini na sita (Tsh 793,553,066) sawa na asilimia 46.

## CHANGAMOTO ZA WIZARA

Wizara ya Utalii na Mambo ya Kale licha ya kufanikiwa katika utekelezaji wa malengo na shughuli zake ilizojipangia, pia, inakabiliwa na changamoto mbali mbali miongoni mwao ni kama zifuatazo : -

I. Ushindani wa biashara ya utalii kutoka nchi zenye bidhaa zinazofanana na Zanzibar. Kama inavyofahamika kwamba utalii ni biashara kubwa duniani ambapo mataifa hushindana katika utoaji wa huduma bora kwa lengo la kuwavutia wageni,nchi yetu imekuwa ikikabiliwa na changamoto hiyo kutoka kwa mataifa yenye mfanano na Zanzibar kama visiwa vya Maldives, Seychelles na Thailand.
II. Uvamizi katika maeneo ya kihistoria yaliyopo nchini. kwa kipindi kirefu maeneo mengi ya kihistoria yaliyopo nchini yalikosa ushughulikiaji wa karibu; hali iliyopelekea wananchi waliopo karibu na maeneo hayo kuyavamia kwa shughuli za kilimo, ufugaji na makaazi,kadhia hii imepelekea kuharibika kwa kasi kwa maeneo hayo pamoja na kupoteza uhalisia na historia ya sehemu husika.
**III.** Ukiukwaji wa masharti ya vibali kwa wamiliki wa nyumba za Mji Mkongwe ambao huzifanyia matengenezo kinyume na vibali walivyoomba. Hali hii hupelekea kupoteza uhalisia wa majengo yaliyomo ndani ya Mji Mkongwe.

## MAONI, USHAURI NA MAAGIZO YA KAMATI

1. Kamati inaipongeza Wizara kwa kuweza kufikia malengo ya ukusanyaji wa mapato waliojiwekea kwa kipindi cha robo mbili (Julai-Disemba) kwa mwaka 2024/2025 kwa kufanikiwa kukusanya Jumla ya shilingi bilioni nne, milioni mia saba kumi na mbili, laki tisa thalathini na mia mbili sitini na saba (Tsh 4,712,930,267/=) sawa na asilimia 166 ya makadirio ya shilingi ya bilioni mbili, milioni mia nane na thalathini na tano na laki nane sabini na mbili ( Tsh. 2,835,872,000/=) Kwa kipindi hicho.

2. Kamati inatoa pongezi hizo kwa Wizara pamoja na Taasisi zake ambazo zimevuka malengo kama vile Kamisheni ya utalii kwa kukusanya mapato kwa asilimia 168%, Mamlaka ya Mji Mkongwe kwa kukusanya mapato kwa asilimia 822% na Makumbusho ya Mambo Kale kwa asilimia 131%.

3. Kwa hatua hiyo kubwa ya kuvuka malengo hayo ya ukusanyaji wa mapato kwa Wizara na taasisi zilipo chini yake, Kamati inaishauri Wizara kuendeleza mashirikiano yake vizuri na taasisi hizo kwa kuzipa miongozo na ushauri mbalimbali katika namna bora ya kubuni vyanzo mbalimbali vya mapato na kusisitiza matumizi ya njia za kielektroniki katika ukusanyaji wa mapato katika taasisi hizo.

4. Kamati imesikitishwa na uingiaji wa fedha za matumizi mengineyo (OC) kwa Wizara ya Utalii ambayo inafanya juhudi kubwa ya kuendeleza miradi mbalimbali ya utalii na kuitangaza Zanzibar nje na ndani ya nchi, Kamati inaishauri Serikali kuipatia fedha kwa wakati na kwa kiwango walichokadiria kukipata kwa kila robo mwaka ili Wizara iweze kutekeleza shughuli zao walizojipangia kwa lengo kuwavutia watalii duniani kuja kutalii Zanzibar na hatimae kuiongezea Serikali yetu mapato yanayotokana na Sekta ya Utalii.

5. Kamati imearifiwa kuwa idadi ya watalii wanaoingia nchini imeongezeka kwa asilimia 14, Kamati inapongeza Wizara kwa jitihada hizo hata hivyo, Kamati inaendelea kusisitiza uharakishaji wa matumizi ya mifumo ya Tehama katika kuwatambua wageni wanaoingia nchini katika maeneo ya uwanja wa ndege na Bandarini kwa vile

mfumo unaotumika sasa hivi hautoi takwimu sahihi za uingiaji wa wageni nchini na kusababisha kuikosesha Serikali mapato.

6. Kamati inaendelea kuipongeza Wizara kupitia Kamisheni ya Utalii kwa kuendelea Kuutangaza Utalii wa Zanzibar kupitia utalii wa Mikutano, Michezo, na kushiriki katika maonesho, na matamasha ya ndani na nje ya nchi. Mbali na hayo Kamati inaishauri Wizara kuwekeza katika Miradi mikubwa ya ujenzi wa kumbi kubwa za kimataifa za mikutano pamoja na viwanja vya michezo vya aina mbalimbali kwa lengo la kuendesha michezo ya Kimataifa pamoja na kupata nafasi ya kuandaa mikutano ya Kimataifa ndani ya Zanzibar ambayo kwa kiasi kikubwa inasaidia katika kuutangaza na kukuza utalii wetu.

7. Kamati inaipongeza Wizara Kupitia kamisheni ya Utalii kwa kupata tunzo ya "Romantic Destination" iliyotolewa na taasisi ya Travel & Leisure ya India. Aidha Zanzibar kutangazwa kuwa Kisiwa Bora cha Pili Duniani kwa Mapumziko ya Watalii, katika mwaka 2024, Hakika hiyo ni juhudi kubwa inayofanywa na Kamisheni ya Utalii kwa kushirikiana na Wizara katika kuutangaza utalii wa Zanzibar, Kamati inaishauri Serikali kuunga mkono Kamisheni ya Utalii katika kuendeleza jitihada zake za kuutangaza utalii wetu katika masoko mbalimbali duniani ili kuleta ushindani kwa mataifa yenye mfanano na Zanzibar kama visiwa vya Maldives, Seychelles na Thailand.

8. Kamati inaigiza Wizara kuharakisha mchakato wa kujenga uzio au fensi katika maeneo yote ya kihistoria ambayo yanakubwa na changamoto ya uvamizi na uharibifu na kuyapatia hati miliki maeneo yote hayo, Kamati inaliagiza hilo kutokana na umuhimu wa maeneo hayo ambayo yana historia kubwa ya nchi yetu. Aidha ni maeneo ambayo yanavutia sana wageni na wenyeji kujifunza historia na mambo ya kale katika visiwa vya Zanzibar na hatimae kupelekea kukua kwa utalii wetu.

9. Kamati inaishauri Wizara kupitia Kamisheni ya Utalii katika kitengo cha polisi utalii na Diplomasia kuwapa mafunzo askari hao ili kutekeleza wajibu wao wa kusimamia ulinzi na usalama katika maeneo mbalimbali ya kitalii nchini, licha ya kuwa ulinzi

unazidi kuimarika wapo baadhi ya askari si waadilifu na wanashiriki katika vitendo vya rushwa, Kamati inaiagiza Wizara kuchuka hatua kali kwa askari yoyote atakaebainika katika kushiriki vitendo hivyo ambavyo vinapelekea kuwakosesha amani na utulivu wageni ambao wanatembelea katika maeneo ya kitalii ikiwemo eneo la Mji Mkongwe.

10. Kwa kua Kamati imearifiwa kwamba Kamisheni ya Utalii imeshakamilisha uandaaji wa Kanuni ya nyumba za kulala wageni, na tayari wana mfumo ambao utawabaini wale wote ambao hawana leseni ya biashara hiyo, Kamati inasisitiza kuanza kwa utekelezaji wa Kanuni hiyo pamoja na mfumo ili kuhakikisha wageni wote wanaoingia nchini wanalala katika makaazi rasmi yaliyopatiwa leseni kwa ajili ya usalama wao pamoja na kudhibiti mapato ya Serikali.

11. Kamati inaipongeza Wizara kupitia Ofisi kuu Pemba kwa kushirikiana na Kamisheni ya Utalii katika kufanikisha kuandaa tamasha la Mswahili wa Pemba, Kutayarisha tamasha la 'Tourisports Bonanza ambalo hufanyika Pemba kila mwenzi Novemba, na kuanza kutayarisha Tamasha la Mswahili wa Unguja, Kamati inaishauri Wizara kushirikiana na wadau pamoja na Sekta binafsi katika kuendeleza matamasha hayo ambayo kimsingi yanautangaza utalii wa Zanzibar ikiwa ni pamoja na historia yake na utamaduni wa watu wa Zanzibar.

12. Katika dhana ya Ushiriki na ushirikishwaji wa wananchi katika Sekta ya Utalii. Kamati inaiagiza Wizara kuendelea kuwapatia mafunzo ya nadharia na vitendo wakiwemo vijana, watu wenye ulemavu, kinamama na kinababa juu ya njia bora za uandaaji wa bidhaa za kitalii zinazotokana na kilimo hai, pamoja na njia bora za kulitumia soko la utalii la Zanzibar kwa lengo la kunufaika na Sekta ya utalii nchini na kujikwamua katika hali ngumu ya kimaisha.

### 4.3 UTEKELEZAJI WA MIRADI YA WIZARA

Wizara ya Utalii na Mambo ya Kale inaendelea na utekelezaji wa mradi wa maendeleo wa "Kuimarisha Maeneo ya Kihistoria". Kwa sasa Wizara ipo katika hatua za utekelezaji wa miradi hiyo ambao ilianzwa kutekelezwa katika bajeti ya mwaka wa fedha 2022/2023. Katika miradi

hii, maeneo yanayofanyiwa matengenezo ni pamoja na eneo la mradi wa eneo la kihistoria la kasri ya mwinyi mkuu-dunga na mradi wa Eneo la Kihistoria la Kasri ya Bi.-Khole Bungi.

### A) Mradi wa eneo la kihistoria la kasri ya mwinyi mkuu-dunga

Kutokana na umuhimu wake mkubwa kihistoria na kiutamaduni Kasri ya Mwinyi Mkuu ilitangazwa rasmi kuwa hifadhi ya urithi wa mambo ya kale katika mwaka 1947 Aidha, katika juhudi za kuhifadhi na kuendeleza urithi wa Mambo ya kale kwa manufaa ya Taifa kihistoria, kiutamaduni na kiuchumi Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar, kupitia mradi wa kuendeleza maeneo ya kihistoria ulio Chini ya Wizara ya Utalii na Mambo ya Kale ililifanyia ukarabati mkubwa wa Kasri hili.

Ukarabati huu ulijumuisha jengo kuu, kisima, hodhi na mahabusu pamoja na kutengeneza bustani na kujenga jengo la huduma. Ukarabati huu ambao uliongeza haiba, uasili, thamani na mvuto wa Kasri kwa jamii na wageni wa ndani na nje ya nchi ulikamilika Novemba 2022 chini ya msimamizi Yassin & Sons Company Limited na uligharimu jumla ya Shilingi milioni mia nane na mbili, laki nne na sabini na nne na mia tatu na nne nukta sita (Tsh. 802,474,304.60) Kukamilika kwa ukarabati huo kumeongeza idadi ya wageni wanaotembelea Kasri hii hususan kutoka ndani ya nchi.

### B) Mradi wa Eneo la Kihistoria la Kasri ya Bi.-Khole Bungi

Kutokana na umuhimu wake mkubwa kihistoria na kiutamaduni Kasri ya Bi. Khole ilitangazwa rasmi kuwa hifadhi ya urithi wa mambo ya kale katika mwaka 2002. Aidha, katika juhudi za kuhifadhi na kuendeleza urithi wa Mambo ya kale kwa manufaa ya Taifa kihistoria, kiutamaduni na kiuchumi Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar, kupitia mradi wa kuendeleza maeneo ya kihistoria ulio Chini ya Wizara ya Utalii na Mambo ya Kale ililifanyia ukarabati mkubwa Kasri hii.

Ukarabati huu ambao uliongeza haiba, uasili, thamani na mvuto wa Kasri kwa jamii na wageni ulikamilika Novemba 2022, chini ya usimamizi wa Azam Contractor. Jumla ya Shilingi milioni mia nane kumi na saba na laki mbili ishirini na sita na mia saba thamanini

na nane nukta tano (Tsh.817,226,788.50) zilitumika katika utekelezaji wa mradi huo. Kukamilika kwa ukarabati huu kumeongeza idadi ya wageni wanaotembelea Kasri hii hususan kutoka ndani ya nchi.

### MAONI, USHAURI NA MAAGIZO YA KAMATI

Kamati ilipata fursa ya kukagua miradi hii miwili ya kuendeleza maeneo ya kihistoria ikiwa ni pamoja na Kasri ya Mwinyi Mkuu- Dunga na Kasri ya Bi.-Khole Bungi na Kutoa maoni yake kama ifuatavyo;

1. Kamati inaipongeza Wizara katika jitihada zake za kuyatunza na kuyaendeleza maeneo haya ya kihistoria ambapo kwa kiasi kikubwa yalikua yameshaanza kupoteza uhalisia wake kutokana na uchakavu. Kamati inaishauri Wizara kuendelea na jitihada zake hizo kwa vile maeneo hayo ni moja kati ya rasilimali kubwa ya kihistoria ambayo tunayo, hivyo hayapaswi kupuuzwa kwa vile ndio tegemeo la kukuza utalii wetu nchini.
2. Kamati imebaini kuwa bado malengo ya kuendeleza miradi hiyo haijafikiwa, hivyo Kamati inaishauri Wizara kushirikiana na Sekta Binafsi katika kuekeza shughuli mbalimbali za kibiashara zikiwemo mikahawa, maduka na ukodishaji wa kumbi za mikutano katika maeneo hayo kwa ajili ya wageni na wenyeji kwenda kuburudika na kujifunza historia ya maeneo hayo.
3. Kamati inaiagiza Wizara kufanya Marekebisho ya Milango katika Majengo ya Bi-Khole ambapo kamati ilipofanya ziara katika eneo hilo imejionea milango hiyo imeshaanza kutoka katika maeneo yake na kupelekea kupoteza mvuto na haiba katika majengo hayo.

### 4.4 KIVUTIO CHA UTALII CHA MTO FURAHA -PEMBA

Wizara ya Utalii na Mambo ya Kale kwa kushirikiana na Jumuiya ya kijani iitwayo 'Pemba Swimming Sport And Marine Development Center' wapo kwenye maandalizi ya mto huo kuweza kutembelewa na wageni wengi na kuiletea tija Serikali na Jamii iliyoizunguka mto huo.

Shughuli mbalimbali zimepangwa kufanyika ili kuwavutia wageni wanaotembelea mto huo ikiwemo;

i. Michezo ya Baharini

ii. Kutembelea ufugaji wa kaa na kamba

iii. Utalii wa Kijiji (kujionea shughuli za ulimaji wa chumvi, upakasaji na shughuli nyenginezo)

iv. Uvuvi wa asili.

## MAONI, USHAURI NA MAAGIZO YA KAMATI

Kamati ilipata fursa ya kutembelea eneo hilo na kutoa maoni, ushauri na mapendekezo yake kama ifuatavyo;

1. Kamati inaishauri Wizara kushirikiana na Jumuiya zinazoshughulikia mto furaha kuutangaza mto huo pamoja na vivutio vyake ndani na nje ya Pemba ili kuweza kuwavutia wageni na wenyeji mbalimbali kwenda kujionea mandhari nzuri wa mto huo pamoja na kushiriki shughuli mbalimbali ambazo zinapatika katika eneo hilo kama vile michezo ya baharini.
2. Kamati inaendelea kuishauri Wizara juu ya kuzisimamia jumuiya hizo kwa kuziunganisha pamoja kwa lengo la kuwa kampuni moja ambayo itaweza kumudu vyema Shughuli za uhifadhi na uendelezaji wa mto huo kibiashara, aidha kitendo hicho kitapelekea kupata msaada wa mikopo kutoka taasisi za kifedha na kuepusha mgongano wa kimaslahi miongoni.
3. Pamoja na Shughuli za kitalii zinakusudiwa kufanyika katika eneo hilo, Kamati inaiagiza Wizara kuhifadhi Mazingira pamoja na uoto wa asili uliopo pembezoni mwa mto huo wakati wageni na wenyeji wanapoenda kutembelea eneo hilo ili kulinusuru eneo hilo na janga la uharibifu wa mazingira
4. Kamati imejionea uwekezaji uliofanywa na taasisi ya Milele Foundation katika eneo hilo ambapo kwa sasa wakaazi kutoka maeneo mbalimbali ya Pemba huvutiwa kwenda kuburudika katika eneo hilo, Kamati inashauri Serikali kuangalia uwezakano wa kumpatia hati ya matumizi ya eneo liliopo pembezoni ya mto huo kwa ajili ya kuliboresha zaidi kwa kuwekeza vivutio mbalimbali kama vile pembea za kufurahishia watoto n.k

## 4.5 MAMLAKA YA MJI MKONGWE.

## 4.6 UKUSANYAJI WA MAPATO

Mamlaka ya Mji Mkongwe kwa kipindi cha robo mbili Julai - Disemba kwa mwaka wa fedha 2024/2025 imekadiria kukusanya jumla ya shilingi milioni mia moja arubaini na nne na laki tisa arubaini na saba (Tsh. 144,947,000) Na kwa kipindi hicho Mamlaka ya Mji Mkongwe imefanikiwa kukusanya jumla ya shilingi bilioni moja milioni mia moja tisini na moja laki nne sabini na mia tatu ( Tsh. 1,191,470,300) sawa na Asilimia 822%

**MATUMIZI YA MAMLAKA YA MJI MKONGWE**

Mamlaka ya Mji Mkongwe kwa kipindi cha robo mbili Julai – Disemba kwa mwaka wa fedha 2024/2025, imekadiria kupokea ruzuku ya shilingi milioni mia tano na arubaini na nne na elfu thamanini na tano (Tsh 544,085,000/=) kwa ajili ya mishahara na zilizopatikana ni shilingi milioni mia nne hamsini na sita, na laki nne arubaini na moja mia sita na saba (Tsh 456,441,607/=) sawa na asilimia 84 Aidha, kwa upande wa matumizi mengineyo Mamlaka imekadiria kutumia jumla ya shilingi milioni mia moja thamanini na saba na laki nane (Tsh 187,800,000/=) kwa kipindi cha robo mbili Julai – Disemba kwa mwaka wa fedha 2024/2025, na kufanikiwa kutumia jumla ya shilingi milioni sabini na saba, laki sita na kumi na mia nne na saba (Tsh 77,610,407/=) sawa na asilimia 41.

**MAONI, USHAURI NA MAAGIZO YA KAMATI**

1. Kamati inaipongeza Mamlaka kwa kuweza kufikia malengo ya ukusanyaji wa mapato ambapo kwa kipindi cha robo mbili (Julai-Disemba) kwa mwaka wa fedha 2024/2025 imekusanya jumla ya shilingi bilioni moja, milioni mia moja na tisini na moja, laki nne sabini na mia tatu (Tsh. 1,191,470,300) sawa na asilimia 822% ya shilingi milioni mia moja arubaini na nne, laki tisa arubaini na saba (Tsh. 144,947,000) ambayo imekadiriwa kukusanywa kwa kipindi hicho, ongezeko hili limetokana na kubadilishwa kwa Sheria ya Mamlaka ambayo imepelekea kuongezeka kwa eneo la Mamlaka ya Mji Mkongwe pamoja na kuogezeka vyanzo vya mapato ambavyo hapo awali vilikuwa vinakusanywa na Baraza la Manispaa ya Mjini kama vile , maegesho ya magari, taka.

2. Kamati inaishauri Mamlaka Katika kuongeza juhudi ya ukusanyaji wa mapato kwa vile maeneo ya Mji Mkongwe ni maeneo ya kitalii na yamejumuisha biashara mbalimbali ndani yake,  hivyo ni wazi kuwa kuna uwanda mpana zaidi wa ukusanyaji wa mapato hasa kwa kutumia mifumo ya kielektroniki ambayo itasaidia katika kudhibiti wa mianya ya upotevu wa mapato.
3. Aidha Kamati inaendelea kuishauri Mamlaka katika utayarishaji wa Bajeti ijayo ya mwaka 2025/2026 kutayarisha makadirio ya ukusanyaji wa mapato kulingana na uhalisia wa makusanyo katika bajeti inayoendelea ya 2024/2025 ili kuepusha tofauti kubwa ambayo imejitokeza kwa sasa baina ya kilichokadiriwa na kilichokusanywa kutokana na kuongezeka kwa vyanzo vya mapato vya Mamlaka ambavyo havikukadiriwa hapo awali wakati wa utayarishaji wa bajeti ya mwaka 2024/2025

### 4.7 UTEKELEZAJI WA MIRADI YA MAMLAKA YA MJI MKONGWE

#### 1a) UKARABATI WA JENGO LA BEIT AL AJAIB

Tunapenda kuishukuru Serikali ya Oman kwa kuingia Mkataba na Kampuni ya Nandhra Engineering & Construction Company LTD tarehe 13/02/2023, kwa ajili ya ukarabati wa kina wa ujenzi huo ambao ulipangwa kukamilika kwa kipindi cha miaka mitatu. Gharama za awali za Mkataba huo ni Dola za Kimarekani Milioni 21.

Hatua ya ukarabati wa jengo hili unaendelea vizuri sana ambapo tayari jengo lote limeekewa vizuizi, ujenzi wa misingi unaendelea na vifaa mbali mbali kwa ajili ya ujenzi vimeanza kuwasili Zanzibar.

Hatua ya kazi kwa sasa imefikia asilimia 34 na fedha zilizolipwa kwa Mkandarasi ni Dola za Kimarekani milioni tatu, laki tisa arubaini na nane elfu na mia sita thamanini nukta tisa ( 3,948,680.90.)

#### 1b) UKARABATI WA JENGO LA PALACE MUSEUM (JUMBA LA WANANCHI)

Jengo hili lipo katika hatua za mwisho la kutengeneza nyaraka za zabuni kwa ajili ya kupelekwa UNESCO ili kupata kibali cha ruhusa cha kutafuta Mkandarasi wa ukarabati wa ujenzi huu. Kazi ya utayarishaji wa Nyaraka hizo ilifanywa na Kampuni ya GMP

kutoka Arusha Tanzania na sasa imewasilishwa kwetu kwa mapitio. Kazi hii pia ipo chini ya udhamini wa Serikali ya Oman.

## 1c) UIMARISHAJI WA MAKUMBUSHO YA MAKABURI YA WAFALME WALIOTAWALA ZANZIBAR

Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kwa kushirikiana na Serikali ya Oman imejenga makumbusho na kuimarisha makaburi yaliyopo pembezoni mwa Jumba la Wananchi. Kazi hiyo iligharimu Dola za Kimarekani (USD) laki moja arubaini na tisa elfu na mia mbili hamsini na tatu (149,253/- ) na imekamilika na kuanza matumizi.

## MAONI, USHAURI NA MAAGIZO YA KAMATI

1. Kamati inaipongeza Serikali kwa jitihada zake kuendeleza mashirikiano na Serikali ya Oman katika kuendeleza Sekta ya utalii nchini kwa kuboresha makumbusho mbalimbali ya falme za kiarabu zilizotawala Zanzibar enzi za ukoloni. Kamati inaishauri Serikali kuendeleza mashiriakiano mema na Serikali ya Oman katika jitihada za kuunga mkono katika kukuza sekta ya utalii nchini husasan katika mambo ya kale ambayo yana mchango mkubwa katika kukuza utalii wa Zanzibar.
2. Kamati inaishauri Wizara kuitunza na kuilinda miradi yote ya Mji Mkongwe iliyofadhiliwa na Serikali ya Oman ambayo imeshakamilika na kuanza kutumika, Kamati inalisisitiza hili kwa vile maeneo hayo yanatembelewa na makundi mbalimbali ya kijamii yakiwemo wanafunzi wa Skuli mbalimbali za ndani na nje ya Zanzibar ambapo kwa bahati mbaya au kwa makusudi husababisha uharibu wa baadhi ya vifaa vilivyomo katika majengo hayo.
3. Kamati ilifanikiwa kutembelea Beit Al Ajaib na kujionea ujenzi ukiendelea licha ya kuwa jumba hilo limechukua muda mrefu kufanyiwa marekebisho yake. Kamati inaisisitiza Wizara kusimamia vyema utekelezaji wa mradi huo ili uweze kukamilika kwa wakati uliopangwa.

## 2a) UKARABATI WA NGOME KONGWE NA JENGO LA CARAVAN SERAI

Wizara ya Utalii na Mambo ya Kale iliingia Mkataba wa Ubia baina yake na Kampuni ya Infinity Foundation ya kulifanyia usafi jengo la Ngome Kongwe katika kuta zote za jengo hilo, kuimarisha na kuboresha miundombinu ya umeme na maji pamoja na kufunga vibanda vya mbao vya biashara vinavyoendana na haiba na maendeleo ya Zanzibar ya sasa.

Makubaliano ya Mkataba huu ni Mjenzi kugharamia ukarabati wote wa jengo pamoja na maboresho yake. Serikali na Muwekezaji watakua na Mgao wa asilimia 50/50. Fedha atakazotumia Muekezaji ni sehemu ya uwekezaji na hazitolipwa wakati wa uendeshaji wa Mradi. Mkataba huu ni wa miaka 25.

Ukarabati huu ulipangwa kukamilika Disemba 2024 ili iwe ni sehemu ya shamra shamra za kusherekea kilele cha sherehe cha Mapinduzi Matukufu ya Zanzibar. Hata hivyo, ujenzi huu utachelewa kukamilika kwakwe hadi mwezi wa Aprili 2025 kutokana na kupisha tamasha la Busara linalotarajiwa kufanyika mwezi wa Febuari 2024 pamoja na kukamilisha ukarabati wa jengo la Caravan Serai.

## 2b) UKARABATI WA MAKUMBUSHO YA MAHAKAMA NA MAHAMAMU YA MJI MKONGWE

Wizara ilipata maelekezo kutoka Serikali Kuu juu ya kufanya mabadiliko ya matumizi ya jengo hili na kulifanya liwe ni makumbusho ya utamaduni pamoja na Mahakama. Kazi hii inaendelea vizuri na ni sehemu ya Mkataba wa Ngome Kongwe. Ukarabati Mkubwa wa Mahamamu yaliyopo Mji Mkongwe ni sehemu ya Mkataba huu.

## 2c) UIMARISHAJI WA BUSTANI YA AFRICA HOUSE

Wizara ya Utalii na Mambo ya Kale kupitia Mamlaka ya Hifadhi na Uendelezaji Mji Mkongwe iliingia Mkataba wa Ubia baina yake na Kampuni ya Infinity Foundation ya kuindeleza bustani hii ili kurejesha haiba ya mji wetu na kuongeza vivutio vya utalii ndani ya eneo la Mji Mkongwe.

Eneo hili litakua na bustani ya kisasa pamoja na kiwanja cha burudani ya mchezo wa Pedacourt. Pia kutakua na mkawa na chelezo ili kujenga mazingira mazuri na salama ya wenyeji na wageni wanaotembelea visiwani. Vile vile eneo hili litakua na boti za kisasa ambazo zitatumika kama taxi za baharini kufuatia maelekezo ya Mheshimiwa Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi ya kutaka kuanzishwa kwa usafiri wa aina hii Zanzibar. Eneo la bustani litakua na uwezo wa kutumiwa na idadi ya watu 500 kwa wakati mmoja. Makubaliano ya Mkataba huu ni Mjenzi kugharamia ukarabati wote wa jengo pamoja na maboresho yake na kuihudumia bustani hii kwa muda wote wa Mkataba. Serikali na Muwekezaji watakua na Mgao wa asilimia 50/50. Fedha atakazotumia Muekezaji ni sehemu ya uwekezaji huo. Mkataba huu ni wa miaka 15.

Mradi huu ulianza tarehe 02/09/2024 na sasa upo asilimia 60.2% na unatemegewa kukamilika tarehe 02/05/2025 na kutumia gharama za Dola za kimarekani laki nane na hamsini ( 850,000/=)

## MAONI, USHAURI NA MAAGIZO YA KAMATI

1. Kamati inaipongeza Serikali kwa kumpata muwekezaji huyu wa Kampuni ya Infinity Foundation ambae uwekezaji wake unaonekana kuleta tija kwa nchi yetu na kuimarisha utalii wetu husasan katika eneo la Mji Mkongwe, Kamati inaishauri Serikali kuunga mkono jitihada za Mwekezaji huyu ikiwa ni pamoja na kumuwekea mazingira wezeshi ili aweze kutekeleza miradi hii kwa ufanisi mkubwa.
2. Aidha Kamati inaipongeza Mamlaka ya Mji Mkongwe kwa kushirikiana bega kwa bega na Mwekezaji huyu katika harakati za uendelezaji wa miradi hiyo, Kamati inaishauri Mamlaka kuendelea kusimamia vyema utekelezaji wa miradi hiyo ili iweze kumalizika kwa wakati na tija iliyokusudiwa iweze kupatikana.

3. Licha ya uendelezaji mzuri wa miradi ya Mji Mkongwe kwa Kampuni ya Infinity Foundation, Kamati inaiagiza Mamlaka kuhakikisha miradi yote hiyo haipotezi uhalisia na uasili wa majengo hayo ya kihistoria ambayo ndio kivutio kikubwa cha utalii nchini.

## 4.8 MIRADI JUMUISHI INAYOSIMAMIWA NA MAMLAKA YA MJI MKONGWE

### UIMARISHAJI WA BUSTANI YA HOSPITALI YA MNAZI MMOJA (TENGA GARDEN)

Tunapenda kutoa shukurani zetu za dhati kwa Mwenyekiti wa Kampuni ya Infinity Foundation ambayo ilitupatia ufadhili wa bustani hii kuanzia michoro hadi ujenzi na kulipa wa gharama zote za mradi huu hadi pale walipoikabidhi kwa Serikali.

Mradi huu ni sehemu moja muhimu iliyobadilisha mandhari ya Mji na Nchi yetu kwa ujumla. Mamlaka imeajiri kampuni makhsusi kuhakikisha ubora wa bustani hii haushuki.

### UPAKAJI WA RANGI MAJENGO YA MJI MKONGWE

Kampuni ya Infinity Foundation imeshasaini MoU na Mamlaka ya Mji Mkongwe ya kufanya zoezi la kupaka rangi majengo yote yaliyomo ndani ya Hifadhi ya Mji Mkongwe.

Mradi huu unategemewa kutumia kiasi kikubwa cha fedha ambazo zote zitagharamiwa na Kampuni hiyo katika kuunga Mkono Juhudi za Mheshimiwa Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi la kutaka kufanya maboresho makubwa na kuupendezesha Mji Mkongwe.

### UKARATABI WA MAJENGO YALIYO KATIKA HALI MBAYA NDANI YA ENEO LA HIFADHI YA MJI MKONGWE

Kwa upande mwengine, Wizara kupitia Mamlaka ya Hifadhi na Uendelezaji Mji Mkongwe inaendelea na kufanyia ukarabati mkubwa wa nyumba za Mji Mkongwe kama vile Ofisi za Mamlaka ya Mji Mkongwe, Jengo la Culture, Jengo la Wizara.

**UFUNIKAJI WA MITARO ILIYOMO NDANI YA HIFADHI YA MJI MKONGWE**

Mamlaka imeshakamilisha taratibu zote za zabuni kwa ajili ya kufunika mitaro yote iliyowazi katika eneo la Mji Mkongwe

**UJENZI WA NJIA ZOTE ZA NDANI YA ENEO LA MJI MKONGWE NA MAENEO YA MAENGESHO.**

Mamlaka imepanga kuziimarisha njia zote za ndani ya maeneo ya Mji Mkongwe na ipo katika hatua za awali za utayarishaji wa zabuni ya kazi hii.

**MAONI, USHAURI NA MAAGIZO YA KAMATI**

1. Kamati inaendelea kuipongeza Mamlaka katika jitihada zake za kuimarisha Mji Mkongwe kwa kuzifanyia ukarabati nyumba ambazo zipo katika hali mbaya ya uchakavu katika eneo hilo, hiyo ni hatua nzuri katika kuutunza Mji huu wa kitalii ambao ni kivutio kikubwa cha utalii na kutuongezea mapato katika nchi yetu. Kamati inaishauri Mamlaka kuendeleza juhudi hizo bila ya kusita ya kuhakikisha majengo yote ambayo yapo katika hali mbaya yanakarabatiwa kwa kurudishwa haiba yake bila ya kupoteza uhalisia wake wa uasili kwa mujibu wa mkataba wa UNESCO.

2. Kamati imearifiwa kuwa zipo baadhi ya taasisi za Serikali na watu binafsi wanakwamisha jitihada za Mamlaka za kuboresha nyumba chakavu ndani Mji Mkongwe kwa kutowakabidhi Mamlaka kwa ajili kuanza ukarabati ambao mmiliki hatoi gharama yoyote.

3. Kamati inaishauri Serikali kuingilia kati jambo hilo kwa kuzitaka taasisi zake pamoja na watu binafsi wanaomiliki nyumba katika eneo la Mji Mkongwe kufuata maagizo yanayotolewa na Mamlaka kwa lengo la kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi mkubwa ya kuutunza na kuuimarisha mji huo ikiwemo kuyakarakabati majengo

ambayo yapo katika hali mbaya ili yasijekuleta athari katika jamii aidha kupoteza haiba na uhalisia ya Mji huo wa Kihistoria endapo yataendelea kuwepo kama yalivyo.

4. Kamati inaiagiza Mamlaka kuharakisha michakato hiyo imalizike kwa haraka ili miradi ianze utekelezaji wake kwa muda uliopangwa na kuweza kukamilika kwa wakati kwa vile mitaro mingi ya Mji Mkongwe haipo salama, inatoa harufu mbaya na huleta kero kwa wanaotembelea katika maeneo hayo hususani watalii na wenyeji.

5. Kamati inaiagiza Mamlaka kuchukua hatua kali kwa wale wote wanakiuka masharti ya vibali kwa wamiliki wa nyumba za Mji Mkongwe ambao huzifanyia matengenezo nyumba hizo kinyume na vibali walivyoomba. Hali hii hupelekea kupoteza uhalisia wa majengo yaliyomo ndani ya Mji Mkongwe na kukiuka masharti ya mkataba wa UNESCO na hatimae Mji huo unaweza kutolewa katika urithi wa dunia.
6. Kamati inaunga mkono hatua za Mamlaka za kusitisha huduma za malazi na hoteli katika nyumba za Mji Mkongwe ambazo zinaendelea kuombewa vibali hivyo, Kamati inalisisitiza hilo kwa vile kuendelea kuwepo kwa hoteli nyingi na mikahawa ndani ya eneo hilo kutasababisha vurugu na kukosa utulivu kwa wageni na wenyeji wanaotembelea katika eneo hilo la kihistoria.

7. Kamati inaendelea kuipongeza Mamlaka kwa kushirikiana na Wizara katika kusimamia utekelezaji wa Miradi inayoendelea katika eneo la Mji Mkongwe kwa kushirikiana na Kampuni ya Infinity Foundation, kwa hakika ushirikiano wenu na Kampuni hiyo kitamuwezesha mwekezaji kutekeleza miradi yake katika eneo hilo kwa ufanisi na hatimae Mji Mkongwe kuwa ni Mji wa Kwanza wa kivutio cha utalii duniani kwa aina ya uwekezaji wake anaotaka kuufanya.

8. Kwa kipekee kabisa Kamati inaipongeza Kampuni ya Infinity Foundation kwa hatua yake ya kuekeza miradi mbalimbali ndani ya eneo la mji Mkongwe ambapo mradi wa Uimarishaji wa Bustani ya Hospitali ya Mnazi mmoja (Tenga Garden) na Mradi

wa Kupanga Rangi Nyeupe Nyumba zote za Mji Mkongwe, miradi yote hii inatekelezwa kwa gharama za Kampuni ya Infinity foundation na hatimae kuikabidhi miradi yote Serikalini ikiwa ni sehemu ya kuunga mkono jitihada za Mhe Rais za kutaka kufanya maboresho makubwa na kuupendezesha Mji Mkongwe.

9. Kupitia Kampuni hii ya Infinity kuonesha nia njema kwa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar Kamati inaiomba Serikali kumpa ushirikiano wa kutosha muwekezaji huyu kwa vile nia yake kubwa ni kuiona Zanzibar inakuwa ni nchi ya kwanza duniani kuwa na vivutio vingi vya utalii ambapo itapelekea wageni wengi kuja kutaalii nchini mwetu hususani katika kupendezewa na haiba nzuri ya Maeneo ya Mji Mkongwe na hatimae kuongeza mapato katika nchi yetu yanayotokana na Sekta ya Utalii.

10. Kamati inaipongeza Wizara kupitia Mamlaka ya Mji Mkongwe katika kufanikisha kuadhimisha Siku ya Mji Mkongwe. Kamati inalipongeza hilo kwa kuamini kuwa maadhimisho hayo yatakuwa yanaendana na uboreshaji wa Mji huo katika kutekeleza Miradi mbalimbali ya kuutunza na kuhifadhi pamoja na kuutangaza nje na ndani ya nchi na hatimae kuongezeka kwa idadi kubwa ya watalii watakao kuja kutembelea Mji huo na kuiongezea Serikali mapato.

## SEHEMU YA TANO

### 5.1 WIZARA YA BIASHARA NA MAENDELEO YA VIWANDA

Wizara ya Biashara na Maendeleo ya Viwanda inaundwa na Idara na taasisi mbali mbali ambazo kwa pamoja zina lenga kutoa huduma kwa wananchi wote bila ubaguzi wowote.

### IDARA ZA WIZARA YA BIASHARA NA MAENDELEO YA VIWANDA

1. Idara ya Uendeshaji na Utumishi

2. Idara ya Sera na Utafiti

3. Idara ya Biashara na Ukuzaji Masoko

4. Idara ya Maendeleo ya Viwanda

5. Afisi ya Afsa Mdhamini Pemba.

### TAASISI NA MASHIRIKA YA WIZARA YA BIASHARA NA MAENDELEO YA VIWANDA

1. Shirika la Biashara la Taifa (ZSTC)

2. Wakala wa Usasjili wa Biashara na Mali

3. Baraza la Taifa la Biashara (ZNBC)

4. Taasisi ya Viwango zanzibar (ZBS)

5. Mamlaka ya Usimamizi wa leseni

6. Wakala wa Maendeleo ya Viwanda Vidogo vidogo, vidogo na vya Kati (SMIDA)

7. Tume ya Ushindani Halali wa Biashara

8. Baraza la Ushindani wa Biashara

9. Wakala wa Vipimo.

Wizara hii katika kutekeleza majukumu yake ya kila siku inajiendesha kupitia Programu kuu zifuatazo:

i. Programu kuu ya ukuzaji na uendelezaji wa biashara

ii. Programu Kuu ya Uendelezaji na Uratibu wa Wizara ya Biashara na Mendeleo ya Viwanda

iii. Programu Kuu ya Viwango na Tathmin na Ubora

**PROGRAMU KUU YA UKUZAJI NA UENDELEZAJI WA BIASHARA**

Programu hii inaundwa na program ndogo zifuatazo:-

i) Programu ya ukuzaji wa masoko na usafirishaji;

ii) Programu ya ushindani halali wa kibiashara na kumlinda mtumiaji;

iii) Programu ya urahisishaji biashara na ukuzaji biashara za ndani;

iv) Programu ya usimamizi wa usajili wa biashara na mali;

**PROGRAMU ZA WIZARA**

Kamati katika kazi zake ilifanya ziara maeneo mbali mbali kwa lengo la kukagua na kujionea hali halisi ya mafanikio na juhudi zinazochukuliwa ambapo, Kamati katika Programu hii ya Ukuzaji na Uendelezaji wa Biashara ilifanya ziara katika maeneo yafuatayo:-

i) Wakala wa Mizani na Vipimo; na

ii) Tume ya Ushindani Halali wa Biashara.

**5.2 WAKALA WA VIPIMO ZANZIBAR**

Wakala wa Vipimo imeundwa kwa mujibu wa Sheria namba sita (6) ya mwaka 2020 kwa madhumuni ya kuhakikisha kuwa vipimo vinakuwa sahihi na vinatumika kama vinavyotakiwa kwa mujibu wa sheria. Kutungwa kwa sheria nambari 6 ya mwaka 2020 ilioanzisha Wakala wa Vipimo kulifuatia baada ya kufutwa kwa Sheria ya Uzito na Vipimo nambari 4 ya mwaka 1983 (Weights and Measures Act, No.4 of 1983). Lengo ni kuhakikisha biashara zinafanyika kwa usahihi baina ya mnunuzi na muuzaji wa bidhaa kwa kutumia vipimo vinavyokubalika.

**MAFANIKIO YA WAKALA WA VIPIMO KWA KIPINDI CHA MWAKA 2023/2024**

i. Kuanza kufanyika kwa kazi ya uhakiki wa gesi inayoingia nchini kupitia bandari ya Mangapwani

ii. Kuenedeleza mashirikiano tulionayo baina ya Wakala wa Vipimo Zanzibar (ZAWEMA) na Wakala wa Vipimo wa Tanzania Bara (WMA) katika kudumisha hati ya makubaliano (MoU), kunakosaidia katika upatikanaji wa uzowefu walionao wenzetu WMA kwenye kazi tunazozifanya.

## CHANGAMOTO

i. Kukosekana kwa Muundo wa Taasisi (ZAWEMA) kulikotokana na kuendelea kwa mchakato wa uunganishwaji wa Taasisi mbili za ZAWEMA na ZBS.
ii. Uhaba wa Maafisa vipimo katika kutekeleza kazi za kila siku za Vipimo unaotokana na kukosekana kwa muundo wa Taasisi utakaopelekea kujulikana kwa uhitaji wa Watendaji katika Idara, Vitengo Pamoja na Divisheni za Taasisi.
iii. Uhaba pamoja na uchelewaji wa uingiaji wa Ruzuku ambao unapelekea Wakala kushindwa kufanya ununuzi wa vifaa pamoja na nyenzo nyengine za kufanyia kazi.
iv. Wakala kushindwa kuhudhuria katika Vikao muhimu vya Kimetrolojia, vinavyofanyika nje ya nchi vikiwemo vya Kikanda pamoja na vya Kimataifa, kutokana na kukosekana kwa fedha ya kutosha katika Bajeti ya Wakala kwa ajili ya kugharamia safari hizo, ambazo nchi washiriki hupaswa kujigharamia wenyewe.

## MAONI, USHAURI NA MAAGIZO YA KAMATI

1. Kamati inaishauri Serikali kuwaingizia ruzuku ya kutosha katika Taasisi hii ili kuiwezesha kutekeleza majukumu yake kwa wakati kwa maslahi ya wananchi na taifa kwa ujumla.

2. Kamati inaishauri Serikali kupitia Wizara ya Biashara ifanye maarifa ya kujenga jengo la ofisi pamoja kuajiri wataalamu wanaoendana na muundo ulioandaliwa na Taasisi.

3. Kamati inaishauri Serikali kupitia Wizara ya Biashara na Maendeleo ya Viwanda kuchukua juhudi za makusudi kuweza kuzipima bidhaa zinazozalishwa nje ya nchi,

kwa lengo la kuweka uwiano ulio sawa na kuondosha migogoro inayojitokeza siku hadi siku miongoni mwa wafanyabiashara.

4. Kamati inaipongeza Wakala wa Mizani na Vipimo kwa mashirikiano yao ya karibu waliyonayo na Wakala wa Vipimo Tanzania Bara.

5. Kamati inaishauri Taasisi hii kushiriki kikamilifu katika siku ya Wakala wa Vipimo duniani, kwa lengo la kuitumia fursa ya kuitangaza taasisi hii na majukumu yake. Kuitangaza Taasisi hii kutatoa fursa Kwa jamii kuielewa vyema na kutoa ushirikiano wa kutosha pale unapohitajika.

## 5.3 TUME YA USHINDANI HALALI WA BIASHARA NA KUMLINDA MTUMIAJI

Programu hii ina jukumu la kusimamia masuala ya ushindani halali wa biashara baina ya wafanyabiashara na makampuni, kuzuia mienendo ya biashara isiyo ya ushindani pamoja na kudhibiti bidhaa bandia katika soko.

### MAFANIKIO YALIYOPATIKANA KATIKA UTEKELEZAJI WA PROGRAMU HII

1. Kupitia Tume ya Ushindani Halali wa Biashara program ndogo ya ushindani halali wa kibiashara na kumlinda mtumiaji kupitia Idara ya Rasiliamali watu Mipango na Utawala imefanikiwa kulipia gharama za stationary,mafuta, internet,kufanya pertition ya ofisi ya Unguja na Pemba, ununuzi wa samani kwa ofisi za Unguja na Pemba.

2. Programu pia kupitia Idara ya Miungano ya Kampuni katika Tume ya Ushindani halali wa kibiashara imefanikiwa kukusanya, kupitia, na kuzifanyia uchambuzi taarifa za maombi ya ununuzi wa hisa za kampuni ya Zantel Telecom Public Limited, Kampuni ya Zantel Mobile Financial Services Solution Limited na Kampuni ya Jubilee General Insurance.

3. Tume kupitia Idara yake ya kumlinda mtumiaji imefanikiwa kukagua maduka 527, maghala 24, Supermarket 2, vyote hivyo ni sawa na asilimia 84.

4. Katika ukaguzi wa maduka uliofanywa na Tume, Tume imefanikiwa kukamata bidhaa za vyakula vya makopo, kemikali, na bidhaa za matumizi ya nyumbani ambazo muda wa matumizi yake umeshapita. Bidhaa hizo zina thamani ya Tsh. **784,000.** Miongoni mwa bidhaa zilizokamatwa ni pamoja na blueband, juisi, soda, sabuni ya unga na pampers.

5. Katika eneo la ukaguzi, Tume imefanikiwa kuwakamata wafanyabiashara **20** wakiuza saruji kinyume na bei elekezi iliyotangazwa na Serikali.

6. Pia Tume ilifanikiwa kukagua mikataba ya watoa huduma **46** na kuendelea na hatua nyengine za kiusajili.

**CHANGAMOTO**

1. Ufinyu wa ofisi ambapo ofisi inayotumika kwa sasa ni ndogo na haikidhi mahitaji.

2. Uhaba mkubwa wa wafanyakazi unaoikabili Taasisi hii ambapo ilielezwa kuwa kwa upande wa Pemba kuna wafanyakazi watano (5) tu ambao kiuhalisia hawawezi kutekeleza majukumu yao kwa ufanisi.

3. Maslahi duni ya wafanyakazi wa Tume ambapo wafanyakazi hao hukumbwa na misuko suko mikubwa pindi wanapotimiza majukumu yao ya kila siku ikiwemo kushambuliwa na baadhi ya wafanyabiashara wanapokutwa na makosa katika bidhaa zao na baadhi ya bidhaa hizo kutakiwa ziangamizwe. Hali hii ni ya kusikitisha sana na haikubaliki hata kidogo.

4. Ukosefu wa usafiri katika Tume ya Ushindani halali wa biashara. Kwa sasa hakuna gari na kazi nyingi za Tume hii zinafanyiika nje ya ofisi na kila Idara inahitaji usafiri ambapo kwa sasa zipo Idara tatu ambazo zinahitaji usafiri katika kutekeleza majukumu yake ya ukaguzi wa bidhaa mbali mbali.

**MAONI, USHAURI NA MAAGIZO YA KAMATI**

1. Kamati inaishauri Serikali kupitia Wizara ya Biashara na Maendeleo ya Viwanda kufanya mipango ya kujenga jengo litakalojumuisha ofisi za Wizara nzima ili matatizo ya ukosefu wa nafasi katika Taasisi nyingi za Wizara hii liweze kuondoka.

2. Kamati inaishauri Serikali kuajiri wafanyakazi wapya wenye utaalamu na vigezo vinavyohitajika ili wafanyakazi hao waweze kutimiza majukumu yao kwa ufanisi pamoja na kuziba pengo kubwa la uhaba wa wafanyakazi liliopo sasa katika ofisi hii.

3. Kamati inaishauri Serikali kuiangalia vyema na kwa umakini miundo ya Taasisi zote za Serikali na iwaongezee maslahi wafanyakazi wake. Kamati inatoa ushauri huu kulingana na kazi kubwa na ngumu wanazozifanya wafanyakazi wetu Serikalini. Aidha, tunaiomba Serikali kwa wale wafanyakazi ambao wana ujuzi adimu Serikali iwaangalie zaidi kwa kuwaongezea maslahi ili waweze kubakia hapa nyumbani na kulijenga taifa letu.

4. Kamati inaishauri Wizara ya Biashara kuipatia Taasisi hii usafiri wa uhakika kwa lengo la kurahisisha utekelezaji wa majukumu yao iliyojipangia hasa tukizingatia kwamba, taasisi hii kazi zake nyingi utekelezaji wake unafanyika nje ya ofisi.

5. Aidha Kamati yetu tunaiomba Serikali kuliangalia upya suala la kubakisha makusanyo yanayokusanywa na taasisi hii japo kwa asilimia Fulani ili baadhi ya changamoto za taasisi iweze kuzitatua yenyewe.

6. Kamati inaishauri Serikali kwa kushirikiana na Wizara ya Biashara na Maendeleo ya Viwanda kuwawekea ulinzi madhubuti wafanyakazi wa Taasisi hii hususani pale wanapofanya ziara ya kukagua katika maduka ya wafanyabiashara ili waweze kufanya kazi zao za ukaguzi kwa usalama zaidi.

### 5.4 TAASISI YA VIWANGO ZANZIBAR (ZBS)

Taasisi ya Viwango Zanzibar (**ZBS**) imeanzishwa kwa mujibu wa Sheria ya Viwango ya Zanzibar Na. **1** ya mwaka **2011.** Majukumu makuu ya Taasisi hii ni (**ZBS**) ni kuandaa Viwango, kuvisimamia na kusimamia ubora wa bidhaa na huduma nchini, bidhaa hizo ziwe zinazozalishwa au kuingizwa nchini kutoka nje ya nchi.

## MAFANIKIO YA TAASISI YA VIWANGO

Taasisi ya Viwango Zanzibar kwa mwaka wa fedha **2023/2024**, ilipangiwa kukusanya jumla ya **Shilingi bilioni saba nukta sifuri moja (Tsh.7.01)** kutokana na vyanzo vyake vya mapato kwa huduma zinazotolewa. Hadi kufikia Juni, 2024 jumla ya **Shilingi bilioni saba nukta mbili saba (Tsh.7.27)** zilikusanywa na kuingizwa katika Mfuko Mkuu wa Serikali ambapo ni sawa na asilimia **104** ya makadirio ya makusanyo.

Taasisi imefanikiwa kupata Ithibati ya Umahiri wa Maabara za ZBS (Accreditation) kwa kutumia kiwango cha ISO/IEC 17025:2017 kutoka kwa Shirika la **SADCAS** ambapo imepelekea majibu ya uchunguzi wa kimaabara za ZBS kuweza kutambulika dunia nzima.

Taasisi imefanikiwa kuratibu kituo cha kisasa cha ukaguzi wa vyombo vya moto kwa kutumia mfumo wa ki electroniki. Mfumo huu utaweza kuisaidia Nchi katika kupata mapato na utasaidia usalama barabarani.

## CHANGAMOTO

Katika ziara hii Kamati ilibaini changamoto zifuatazo:-

1. Ufinyu wa ofisi kwa maeneo yote ya Wete, Chake chake na Mkoani.

## MAONI, USHAURI NA MAAGIZO YA KAMATI

1. Kamati inaishauri Serikali kuharakisha ujenzi wa ofisi za **ZBS** kwa upande wa Pemba ili waweze kueka maabara za vipimo kwa bidhaa ambazo zitaingia Pemba.

2. Taasisi ya ZBS iangalie utaratibu wa kukaa na Wizara ya Fedha ili wapatiwe utaratibu wa kupatiwa mkopo kwa lengo la kujenga jengo lao kwa haraka. Kwa kufanya hivyo, itasaidia kupunguza ucheleweshaji wa uingizaji wa Biashara kwa upande wa Pemba.

3. Kamati inaishauri Taasisi ya **ZBS** kuachana na Utaratibu wa kuruhusu uingiaji wa mizigo kwa njia ya masharti maalumu (**Conditional release**) kwa wafanyabiashara wanaoingiza mzigo nchini. Kwani tumebaini kuwa utaratibu huu unaweza kutoa mwanya kwa wafanya biashara ambao sio waaminiifu kuweza kukiuka mashari wanayopewa na hatimae kuingiza bidhaa hizo sokoni ambazo hazijathibitishwa na kupata ruhusa ya ZBS. Serikali ianzishe utaratibu mpya na wa kisasa ili sampuli isikae sana maabara ikapelekea mizigo kubakia Bandarini.

4. Aidha kamati inaishauri ZBS kuharakisha upatikanaji wa Ghala ambalo mizigo yote inayotolewa kwa masharti maalum (**Conditional release**) itawekwa ili kusubiria matokea ya vipimo kutoka maabara za ZBS kabla ya kuwaruhusu wafanyabiashara kuzitumia bidhaa hizo na kuziingiza sokoni.

5. Tunaishauri Taasisi ya ZBS kuongea na wafanyabiashara pamoja na wajasiriamali kuanzisha utaratibu wa kueka alama za ubora ambazo ni rahisi kuonekana na watumiaji wa bidhaa hizo kwani alama zinazoekwa hivi sasa ni ndogo sana na sio rahisi kwa mtumiaji kuweza kuziona katika bidhaa anazozitumia.

6. Kamati inaishauri ZBS kuanzisha idara ya tafiti na mafunzo kwa lengo la kuboresha tafiti na kutoa mafunzo kwa taasisi za umma na binafsi juu ya kazi za ZBS.

7. Kamati inaishauri Taasisi ya ZBS kuanzisha utaratibu wa kuwasaidia kupata taaluma ya masoko kwa wajasiriamali wadogo wadogo ambao bidhaa zao zimekidhi viwango vya kimataifa. Kwa kufanya hivyo itasaidia kuongeza ukubwa wa soko kwa bidhaa zinazozalishwa nchini.

8. Kamati inaishauri Taasisi hii ya ZBS kufanya utaratibu wa kueka vyombo vya usafiri katika vituo vyao vya kazi viliopo Bandarini na Kiwanja cha ndege. Kwa kufanya hivyo itaharakisha upatikanaji wa majibu kwa sampuli ambazo zinaingia katika bandari na

viwanja vyetu vya ndege. Kwa sasa Vituo hivyo vinategemea gari kutoka Ofisi kuu ambayo muda mwingi haipo katika vituo hivyo.

**9.** Aidha Kamati inaishauri ZBS kuhakikisha maabara nyengine zilizobakia zinafanyiwa tathmini na kuomba ithibati za ubora kutoka **SADCAS** kwa haraka.

## 5.5 KAMPUNI YA MWANI (ZASCO)

Kampuni ya Mwani Zanzibar katika mwaka wa fedha 2024/2025 iliendelea kutekeleza majukumu yake kwa kuzingatia mpango mkakati wake wa mwaka 2023/2028 sambamba na Mpango wa Biashara wa miaka mitano 2023/2028. Aidha utekelezaji huo umezingatia mambo yafuatayo.

1. Ujenzi wa Kiwanda cha Kusarifu mwani
2. Biashara ya Mwani, Programe hii Biashara ya Mwani inajumuisha Ununuzi wa mwani, Uuzaji wa mwani, Gharama za uendeshaji katika biashara ya mwani.
3. Utawala na Uendeshaji wa Kampuni ya Mwani

## CHANGAMOTO

1. Uhaba wa watendaji katika Kampuni. Kampuni ya Mwani tayari inatekeleza Muundo wake wa Taasisi ambao umebainisha Vitengo na Kada mbalimbali. Hivyo, changamoto ya kutokuepo watendaji wa kutosha ni kikwazo kwa Taasisi hii.

2. Ukosefu wa vyombo vya usafiri. Kampuni inakabiliwa na changamoto za usafiri ikiwemo gari kwa ajili ya ufuatiliaji na usafirishaji wa mwani. Kutokana na hilo, Kampuni inalazimika kukodi gari au kutumia gari binafsi za watendaji wa Kampuni kwa ajili ya kufanikisha utekelezaji wa majukumu yake. Hali hiyo inapelekea kuongezeka kwa gharama za uendeshaji wa Kampuni.

3. Kutokuwa na nafasi ya kutosha kwa ajili ya Ofisi Pemba. Kampuni ya Mwani kwa upande wa Pemba bado haina nafasi ya kutosha kwa ajili ya watendaji wake. Hali hiyo inapelekea watendaji kufanya kazi katika mazingira yasiyokuwa rafiki na kunapelekea kupunguza ufanisi.

4. Nafasi finyu na uchakavu wa maghala ya kuhifadhia mwani. Kampuni ya Mwani inahifadhi mwani katika maghala ya kukodi ya Shirika la Taifa la Biashara Zanzibar.

MAONI, MAAGIZO NA USHAURI WA KAMATI

1. Kamati inaipongeza Kampuni kwa kuwasilisha hoja ya kupatiwa watendaji kwa mujibu wa Muundo wa Kampuni. Hatahivyo, tunashauri kuharakishwa kwa mchakato huo ili Kampuni iweze kufanya kazi zake kwa ufanisi.

2. Kampuni ya Mwani ifanye utaratibu wa kuiandikia Wizara ya Fedha na mipango ombi la kupatiwa vyombo vya usafiri ili waweze kutekeleza majukumu yao kwa uweledi na kuachana na tabia za kuazima gari kutoka kwa Wabia wake. Kampuni lazima ijitegemee kwa kila idara ili iweze kutimiza malengo yake.

3. Kamati inaishauri Wizara ya Biashara na Viwanda kutafuta utaratibu mzuri wa kutatua changamoto ya Ofisi kwa Kampuni ya mwani, kwani hivi sasa Kampuni inakodi ofisi na gharama za kodi ni kubwa hasa ukizingatia kamapuni bado ni changa na haijaanza kufanya kazi zake kama ilivyojipangia.

4. Kamati inatoa pongezi kwa Kampuni ya Mwani kwa jitihada walizozionesha za kufanya mawasiliano na Shirika la Taifa Biashara la Zanzibar (ZSTC) na kujadiliana namna ya kufanya marekebisho kwa maghala ambayo yanahitilafu.

## 5.6 KIWANDA CHA KUKAMULIA MAFUTA YA MIMEA PAMOJA NA SHAMBA LA MIKARATUSI TUMBE NA KISHINDENI.

Mikaratusi katika sehemu nyengine duniani imekuwa chanzo kikubwa cha uchumi kutokana na ukuaji wake wa haraka na kuwa na matumizi mengi. Hata hivyo, kamati imetoa ushauri kwa Wizara kufanya utafiti ili kubaini madhara ambayo yanaweza kupatikana kwa kilimo hicho kwani kuana tetesi kwamba baadhi ya mikatusi inaharibu mazingira.

## CHANGAMOTO

1. Kamati imebaini shughuli zinazofanyika katika maeneo ya uzalishaji wa mikaratusi bado sio rafiki kwa watendaji kwani hakuna sehemu za huduma za kijamii na hata usalama wa mali za watendaji kwavile hakuna ofisi wala eneo la mapumziko kwa wanaofika katika eneo hilo.
2. Kukosekana kwa uzio katika maeneo ya mitambo ya uzalishaji wa mafuta.
3. Kutoshirikishwa kikamilifu wananchi waliozunguka maeneo ya mradi.

## MAONI, USHAURI NA MAAGIZO YA KAMATI

1. Kamati inashauri eneo liendelee kupandwa miti ili kusaidia uzalishaji uwe mkubwa.

2. Shirika la ZSTC lijenge utaratibu wa kuwashirikisha wananchi wa maeneo ya jirani pindi wanapotaka kufanya miradi. Kwa kufanya hivyo, uwajibikaji wa wananchi utapatikiana kwavile watahisi na wao ni sehemu ya mradi huo.

3. Tunalipongeza Shirika kwa jitihada zake za kuboresha mazingira hasa kwa yale maeneo ambayo mazingira yaliharibiwa kutokana na shughuli za ki binaadamu kama vile kuchota mchanga au kukata miti kwa ajili ya mkaa na kuni.

4. Kamati inashauri kujengwa uzio katika maeneo ya mitambo ya uzalishaji wa mafuta ya mikaratusi ili kunusuru uvamizi wa maeneo ya viwanda.

## 5.7 BARAZA LA UDHIBITI WA MFUMO WA UTOAJI WA LESENI (BLRC)

Baraza la Udhibiti wa Mfumo wa Utoaji wa Leseni (BLRC) katika mwaka wa fedha 2024/2025 limeendelea kutekeleza majukumu yake kwa kuzingatia mkakati wake, mpango mkakati 2022/2027, Mpango wa Taifa wa Maendeleo na Ilani ya Uchaguzi ya CCM ya mwaka 2020/2025.

### MAFANIKIO YA TAASISI

1. Baraza limefanikiwa kuboresha mifumo ya udhibiti kwa kufanya mapitio ya kanuni za mamlaka za leseni na kutoa mapendekezo yake, kupunguza, kuongeza na kuunganisha kwa baadhi ya leseni hasa kwa zile ambazo msingi wake ni mmoja.

2. Baraza limefanya ukaguzi kwa mamlaka za leseni kwa upande wa Unguja na Pemba.

3. Baraza limefanikiwa kukaa na wadau na kufanya majadiliano juu ya utatuzi wa changamoto baina ya mamlaka na wafanya biashara.

4. Baraza limefanikiwa kuimarisha mifumo yake ya huduma kwa njia za ki elektroniki.

5. Kufanya utafiti juu ya mazingira wezeshi kwa wafanya biashara pamoja na kuimarisha Ofisi na kuwajengea uwezo watendaji.

### CHANGAMOTO

1. Uhaba wa watendaji, baraza linahitaji kuengeza idadi ya kuajiri watendaji wenye utaalamu kwa lengo la kutekeleza majukumu yalioanishwa katika Muundo.
2. Uchakavu wa jengo na vifaa vya Ofisi.
3. Kutopata mashirikiano kwa baadhi ya Mamlaka.

**MAONI, USHAURI NA MAAGIZO YA KAMATI**

1. Kamati inaishauri Wizara kufanya utaratibu wa kuengeza watendaji kwa Baraza la Leseni hasa kwa vile linaenda kua Mamlaka hivyo, watahitaji watendaji wenye uwezo ambao wataweza kusaidia majukumu ya Ofisi hii.

2. Ofisi itafute eneo ili waweze kujenga jengo la Ofisi kwa vile jengo wanalotumia hivi sasa haliendani na hadhi ya chombo hiki.
3. Baraza lifanye marekebisho ya Sheria ili kuleta ufanisi na kuongeza utendaji wa kazi zao za kila siku.
4. Taasisi za Serikali zitoe ushirikiano kwa Baraza la leseni kwa kuwa wao ndio wasimamiaji wakuu wa utoaji wa leseni kwa mujibu wa sheria.

## SEHEMU YA SITA

## 6.1 WIZARA YA KILIMO UMWAGILIAJI, MALIASILI NA MIFUGO

Wizara ya Kilimo, Umwagiliaji, Maliasili na Mifugo inaundwa na Idara na taasisi mbali mbali ambazo kwa pamoja zina lenga kutoa huduma kwa wananchi wote bila ubaguzi wowote.

### IDARA ZA WIZARA YA KILIMO, UMWAGILIAJI, MALIASILI NA MIFUGO

1. Idara ya uendeshaji na Utumishi
2. Idara ya Mipango, Sera na Utafiti
3. Idara ya Kilimo na Uhakika wa Chakula
4. Idara ya Umwagiliaji Maji
5. Idara ya Misitu
6. Idara ya Maendeleo ya Mifugo
7. Afisi ya Afsa Mdhamini –Pemba

### TAASISI ZA WIZARA YA KILIMO, UMWAGILIAJI, MALIASILI NA MIFUGO

1. Taasisi ya Utafiti wa Kilimo
2. Wakala wa Matrekta na Zana za Kilimo

Katika utekelezaji wa majukumu yake ya kila siku Wizara ya Kilimo, Umwagilaji, Maliasili na Mifugo inajiendesha kupitia programu kuu tano ambazo ni:

1. Programu Kuu ya Maendeleo ya Kilimo;

2. Programu Kuu ya Maendeleo ya Rasilimali za Misitu;

3. Programu Kuu ya Maendeleo ya Mifugo; na

4. Programu Kuu ya Uendeshaji na Uratibu wa Wizara ya Kilimo.

**PROGRAMU KUU YA MAENDELEO YA KILIMO**

Programu hii inajumuisha programu ndogo tano ambazo ni;

i) Programu ndogo ya Kuendeleza miundombinu ya umwagiliaji maji,

ii) Programu ndogo ya Utafiti na Mafunzo ya Kilimo,

iii) Program ndogo ya Maendeleo ya Huduma za Kilimo na uhakika wa chakula

iv) Programu ndogo ya uhakika wa chakula na lishe;

v) Programu ndogo ya huduma za Matrekta na zana nyengine za kilimo.

**PROGRAMU ZA WIZARA.**

Kamati katika kazi zake ilifanya ziara katika maeneo mbali mbali kwa lengo kufatilia programu za wizara pamoja na kufanya ziara katika miradi ili kuona mafanikio na juhudi

zinazochukuliwa katika kuwasaidia wananchi ambapo Kamati ilifanya ziara katika maeneo yafuatayo:-

I. Ziara ya Kamati katika chinjio la Kisakasaka Unguja.
II. Kamati ilifanya ziara katika idara ya umwagiliaji Pemba
III. Wakala wa Serikali wa huduma za Matrekta na Zana za Kilimo;
IV. Shamba la malisho ya wanyama;
V. Kituo cha Utafiti wa Kilimo Kizimbani Unguja;
VI. Ziara katika kiwanda cha Minjingu Arusha
VII. Kamati ilikutana na mabibi na mabwana shamba kwa Unguja na Pemba;
VIII. Kamati ilifanya ziara ya kukagua mradi wa ujenzi wa bonde la Cheju B na Kilombero kwa Unguja.

## 6.2 KITUO CHA UTAFITI WA KILIMO KIZIMBANI UNGUJA

Taasisi ya Utafiti wa Kilimo Zanzibar (Zanzibar Agricultural Research Institute -ZARI) ni Taasisi iliyoundwa kwa Sheria No. 8 ya mwaka 2020. Jukumu mama la Taasisi hii ni kufanya, kuratibu, kupanga na kusimamia kazi zote za tafiti zinazohusiana na Kilimo na Maliasili pamoja na kutoa matokeo yake kwa walengwa wakiwemo wakulima na wadau mbalimbali. Ofisi kuu ya ZARI kwa Unguja ipo Kizimbani Wilaya ya Magharibi 'A' na Pemba Matangatuani Wilaya ya Micheweni.

Aidha, Taasisi ina vituo vidogo vidogo vya utafiti katika maeneo mbalimbali ya Unguja na Pemba ikiwemo Kijichi, Selem, Bambi na Makunduchi kwa Unguja na Wesha, Weni, Tumbe na Fundo kwa Pemba.

**MAFANIKIO YALIYOPATIKANA KATIKA TAASISI YA ZARI**

Kupitia mashirikiano na wadau mbali mbali wa maendeleo kama vile "World Vegetable Centre" Taasisi ya ZARI imeweza kufanya uchunguzi wa afya ya udongo kwa maeneo mbalimbali ya Unguja na Pemba. Jumla ya wakulima 500 (Unguja 300, Pemba 200) walipata huduma ya kuchunguzwa afya za udongo katika mashamba yao na kupewa matokeo na ushauri.. Mwaka 2023/2024 Taasisi imeweza kuchapisha na kutoa vitabu vyenye taarifa na matokeo ya tafiti zilizokamilika ili zisambae ndani na nje ya Zanzibar kwa faida ya jamii ya watafiti na wakulima wa maeneno mengine duniani.

**CHANGAMOTO**

I. Wizi na uharibifu wa mali na tafiti za Taasisi

II. Uchakavu wa miundombinu ya utafiti

III. Hali mbaya ya mashamba ya uzalishaji (mashamba ya mikarafuu yamezidiwa na gugu) Pamoja na kwamba mapato ya mashamba haya yanakusanywa na Ofisi ya Msajili wa Hazina, Bado utunzaji wake upo chini ya Taasisi.

IV. Uhaba wa Wataalamu wa Bioteknolojia, Udongo (Soil Science), maradhi ya Mimea (Pathology), Wadudu (Entomology), udhibiti wa Magugu (Weed Management) na Uzalishaji Mbegu (Breeding).

V. Uchakavu wa vifaa vya maabara ya Afya ya Udongo na Maabara ya kuzalisha mimea (Tissue culture).

**MAONI, USHAURI NA MAAGIZO YA KAMATI**

I. Kamati inashauri uongozi wa Taasisi ya ZARI wajenge utaratibu wa kuishirikisha jamii iliyowazunguka katika suala la ulinzi shirikishi ili kupunguza uhalifu unaoendelea kufanyika katika kituo hicho.

II. Kamati inaishauri Ofisi ya Rais Fedha na Mipango kuingiza fedha za uendeshaji wa ofisi (OC) kwa ukamilifu ili waweze kufanya maboresho ya miundombinu yote ambayo inatumika kwa kazi za utafiti kituoni hapo.

III. Kamati inaishauri Wizara ya kilimo kuboresha maabara hizi ili wakulima wetu waweze kupatiwa mbinu sahihi ya kudhibiti mmomonyoko wa udongo, kulinda ardhi, kudhibiti mboji kwenye udongo na matumizi stahiki ya virutubisho, mbolea na umwagiliaji.

IV. Kamati inaishauri Wizara ya Kilimo, Umwagiliaji, Maliasili na Mifugo Kilimo kufanya maboresho kwa kununua vifaa vipya vya maabara ya Afya ya udongo na vifaa vya maabara ya kuzalisha mimea.

V. Kamati inaishauri Wizara ya Kilimo kuomba kibali cha ajira kwa lengo la kuongeza wataalamu wa fani ambazo zinakosekana katika taasisi ya ZARI.

VI. Kamati inaishauri Taasisi ya ZARI ijenge tabia ya kutangaza matokeo ya Tafiti kupitia vyombo vya habari ili wananchi waweze kufaidika na Tafiti hizo.

### 6.3 CHINJIO LA KISAKASAKA UNGUJA

Chinjio la mifugo Kisakasaka ni moja kati ya machinjio yetu muhimu yaliyojengwa tokea enzi za utawala wa Kikoloni wakati Zanzibar na vitongoji vyake vikiwa vidogo zaidi, vyenye wakaazi kidogo na mahitaji ya nyama yakiwa madogo sana ambapo uchinjaji wa ng’ombe na mahitaji ya nyama yalikuwa pia ni madogo. Chinjio hili limekuwa likifanyiwa ukarabati kila baada ya muda kulingana na mahitaji.

Chinjio la Kisakasaka hapo awali lilikuwa chini ya usimamizi wa Wizara ya Kilimo Umwagiliaji Maliasili na Mifugo kupitia Idara ya Maendeleo ya Mifugo, lakini mnamo mwaka 2017 usimamizi ulihamishiwa Baraza la Manispaa ya Magharibi "B" baada ya kuanza utekelezaji wa dhana ya Ugatuzi. Hata hivyo, pamoja na kuondoshwa kwa ugatuzi bado usimamizi wa chinjio hili umebakia chini ya Baraza la Manispaa ya Magharibi B', ambapo utoaji wa huduma za ukaguzi wa nyama unafanywa na Wakala wa Chakula, Dawa na Vipod ozi (ZFDA).

**CHANGAMOTO**

I. Mazingira hayaridhishi kwa kuzalisha nyama kwa afya ya walaji sambamba na mazingira hatarishi kwa wakaazi waliovamia karibu na eneo la machinjio;
II. Ukosefu wa uzio kulizunguka chinjio (fence);
III. Chinjio linao uwezo mdogo wa kuchukuwa ng'ombe si zaidi ya ishirini na tano kwa wakati mmoja hivyo, kwa kipindi cha Siku kuu au siku za mahitaji makubwa linasababisha usumbufu; na
IV. Uchakavu wa jengo na miundombinu ya kuweka mifugo.

**MAONI, USHAURI NA MAAGIZO YA KAMATI**

I. Kamati inashauri Wizara kuboresha mazingira ya vyoo, sakafu, kuta na kuezeka Chinjio hilo kwa lengo la kulinda afya za watumiaji wa chama nchini.

II. Kamati inashauri kuwekwa kwa uzio wa chinjio hilo.

III. Kamati inaishauri Wizara kuharakisha ujenzi wa chinjio jipya ambalo litaweza kuhudumia idadi kubwa ya ng'ombe watakaochinjwa kwa pamoja kulingana na mahitaji

IV. Kamati inashauri Wizara kuboresha jengo pamoja na miundombinu yaliyomo katika chinjio hilo.

**6.4 SHAMBA LA MALISHO YA WANYAMA.**

Shamba la mbegu na malisho ya mifugo Kizimbani ni shamba la Serikali linalomilikiwa na Wizara ya Kilimo, Umwagiliaji, Maliasili na Mifugo na kusimamiwa na Idara ya maendeleo ya mifugo Zanzibar.

Shamba hilo lilianzishwa mnamo mwaka 1979 kwalengo ya kuwa kituo cha uzalishaji wa mbegu za malisho ya mifugo chini ya ufadhili wa Shirika la Chakula na Kilimo la Umoja wa Mataifa (FAO) ambapo hapo awali ilikuwa ni sehemu ya shamba la Ng'ombe wa maziwa katika eneo hili la Kizimbani.

Wizara ya Kilimo, Umwagiliaji Maliasili na Mifugo, kupitia Idara yake ya Maendeleo ya Mifugo, imekuwa ikigawa mbegu hizi bure kwa wafugaji wa ng'ombe wa maziwa ikiwa ni jitihada ya kuhakikisha malisho haya yanasambaa kwa kasi kubwa kwa wafugaji wetu kwa lengo la kupunguza au kuondosha changamoto za malisho ya mifugo (ng'ombe na mbuzi).

## CHANGAMOTO

I. Uhaba wa pembejeo za kisasa za kulimia ikiwemo trekta la uhakika, mashine za kupandia na kupalilia
II. Ukosefu wa miundombinu ya umwagiliaji kwani shamba linategemea misimu ya mvua tu.
III. Uharibifu wa malisho kwa kuingizwa kwa wanyama kutokana na kuchakaa kwa uzio unaozunguka shamba.

## MAONI, USHAURI NA MAAGIZO YA KAMATI

I. Kamati inaishauri Idara ya Maendeleo ya Mifugo kutenga fedha za OC ili kuzidisha uzalishaji wa majani ya aina ya Juncao. kwani imegundulika kua "Nyasi hii ni rahisi kupanda na ina mazao mengi, na kiwango chake cha Protini kinakadiriwa kuwa asilimia 18.6, hivyo faida kubwa itapatikana kupitia nyasi za aina hii.
II. Kamati inaishauri Idara ya Maendeleo ya Kilimo kuandaa miradi ikiwemo wa teknolojia ya 'Juncao' ili uweze kuwafikia wafugaji ambao wanakosa chakula kizuri kwa mifugo yao.

III. Kamati inaishauri Wizara ya Kilimo kuwatumia wataalamu wake kushuka kwa wafugaji na kuwapatia Elimu juu ya ulimani wa nyasi hizo za Juncao.

IV. Kamati inaishauri Wizara ya kilimo kujenga uzio katika mashamba ya malisho ya mifugo ili kuzuia uvamizi unaofanywa na watu kwa kuingiza wanyama katika mashamba yao.

## 6.5 BONDE LA UMWAGILIAJI MAJI LA CHEJU B

Kamati pia ilifanya ziara katika Bonde la Cheju B Lengo ni kufuatilia muendelezo wa utekelezaji wa miradi ya umwagiliaji maji. Kamati ilipowasili katika eneo imekuta ujenzi wa miundombinu kwa hekta 300 unaendelea katika bonde la Cheju B'. Miundombinu hii itaongeza tija katika uzalishaji wa mpunga kufikia uzalishaji wa wastani wa tani 3 - 5 kwa hekta kwa msimu na tani 8 - 11 kwa hekta kwa mwaka, mategemeo ni kufikia tani 15 kwa mwaka.

Ushirikiano mkubwa uliopo baina ya wananchi na Wizara hasa wananchi wa Cheju ambao wamekua wa kiulinda mradi huo kupitia elimu waliyoipata kuhusiana na umuhimu wa mradi na kuamua kuweka ulinzi katika maeneo yote ya utekelezaji wa mradi.

## CHANGAMOTO.

Baadhi ya wakulima wamekataa kuekewa miundombinu ya kisasa ambayo itaenda sambamba na mradi huo.

## MAONI, USHAURI NA MAAGIZO YA KAMATI

I. Kamati inaishauri serikali kupitia Wizara ya Kilimo, kuendelea kuwapatia elimu wananchi wetu juu ya umuhimu wa uwepo wa miradi hii kwa maendeleo yao na taifa kwa ujumla.

II. Kamati inaishauri Wizara kwa kushirikiana na watu wa mradi kuanzisha kamati maalumu ya ulinzi shirikishi itakayosaidia kuyalinda na kuyahifadhi na uharibifu maeneo yote ya mradi ili kupeleka mbele kasi ya maendeleo kwa miradi hii na kuiwezesha kumalizika kwa wakati uliopangwa.

III. Kamati inawapongeza wakulima wote kwa ushirikiano mkubwa walioutoa ili kupisha mradi huu ufanyike katika maeneo ambayo walikua wakiyatumia kwa shughuli zao za maendeleo.

IV. Kamati inaopongeza Kamati ya Ulinzi na Usalama ya Wilaya ya Kaskazini 'B' kwa kuonesha utayari wa kuilinda miradi ya Serikali ambayo imegharimu fedha nyingi sana katika utekelezaji wake.

## 6.6 USIMAMIZI WA MASHAMBA YA KILIMO KWA MABIBI NA MABWANA SHAMBA CHANGAMOTO

I. Kamati ilielezwa kuwa baadhi ya mabibi na mabwana shamba walipatiwa elimu ya kuwasaidia wakulima jinsi ya kulima kilimo chenye tija.

II. Mabibi na Mabwana shamba walipata fursa ya kujadiliana matatizo yao mbele uongozi wa Halmashauri zao na matatizo hayo yalifanyiwa kazi.

III. Kwa upande wa Pemba, Mabibi na Mabwana shamba walifanikiwa kupata ofisi ambazo walikua wakizitumia katika utekelezaji wa majukumu yao ya kila siku.

IV. Mabibi na Mabwana shamba waliieleza Kamati kuwa walifanikiwa kupata vitendea kazi ambavyo viliwasaidia kwa wakati huo kutekeleza majukumu yao kwa ufanisi.

## MAONI, USHAURI NA MAAGIZO YA KAMATI

I. Kamati inaishauri Wizara kuwahamasisha mabibi na mabwana shamba kuandaa mpango kazi utakaowaongoza katika kutekeleza majukumu yao ya kila siku na hatimae kuweza kujifanyia tathmini wao wenyewe juu ya mpango kazi huo.

II. Kamati inaishauri Wizara kuwapatia motisha mabibi / mabwana shamba kwa lengo la kuwaongezea ari ya kufanya kazi pamoja na kuwapa fedha ya mafuta/nauli ili waweze kufanya kazi zao kwa wakati katika hayo maeneo watakayoweza kutafanyia kazi.

III. Kamati inawashauri mabibi na mabwana shamba kuendelea kuwa wazalendo katika kazi zao na waendelee kuwahudumia wakulima kwa kuwapatia elimu stahiki.

## 6.7 KIWANDA CHA MINJINGU ARUSHA

Kamati ya Utalii, Biashara na Kilimo ilifanya ziara mwezi Novemba 10, 2024, iliyoratibiwa na Mamlaka ya Udhibiti wa Mbolea Tanzania (TFRA), iliyolenga kujengea uelewa kwa wajumbe na kuwafunza namna bora inayotumika katika kuzalisha mbolea kwa kuzingatia usalama wa mazingira na kuimarisha afya ya udongo.

Ziara hiyo imefanyika ikiwa ni mkakati thabiti wa Wizara ya Kilimo zanzibar kuongeza matumizi sahihi ya mbolea kwa wakulima wa Zanzibar ili kuongeza tija na uzalishaji utakaoleta usalama wa chakula nchini Zanzibar.

lengo la Wizara ya Kilimo, Mifugo, Umwagiliaji, Mali asili na Mifugo Zanzibar ni kupunguza uagizaji wa mbolea za kemikali viwandani kwa zaidi ya asilia 50 kuanzia Januari mwaka 2025''

## MAFANIKIO YA ZIARA.

Wizara ya Kilimo, Mifugo, Umwagiliaji, Mali asili na Mifugo Zanzibar , imejiandaa kutoa bure Maghala manne kwa kampuni ya Minjingu ili kuhifadhi mbolea na kurahisisha

upatikanaji na usambazaji wa mbolea hiyo mjini Zanzibar kabla ya Mwezi Januari Mwaka 2025.

## MAONI, USHAURI NA MAAGIZO YA KAMATI

1. Kamati ya Utalii, Biashara na Kilimo ya Baraza la wawakilishi Zanzibar inaishauri Wizara ya Kilimo, Mifugo, Umwagiliaji, Maliasili na Mifugo ya Zanzibar kuharakisha mchakato wa kuingia makubaliano na Kampuni ya Mbolea Minjingu inayozalisha mbolea asilia ili kuounguza uagizwaji wa mbolea nje ya Nchi.
2. Kamati inatoa pongezi kwa Wizara kwa kufanya mawasiliano yenye tija na kiwanda cha mbolea kilichopo Arusha (Minjingu)na hatimae kufanikisha Kiwanda kufungua tawi lake hapa Zanzibar kwa lengo la kuwahudumia wakulima wetu.

## 6.8 KIKUNDI CHA UFUGAJI WA NG'OMBE WA KISASA MPAPA.

Kamati ilifanya ziara yake katika kikundi hiki kilichopo Mpapa Mwendapole na kujionea hali halisi ya wafugaji hao, ambao kwa kiasi kikubwa wamefanikiwa katika ufugaji wao. Hatahivyo, Kamati inaamini kuwa kuna changamoto nyingi sana zinazowakabili wafugaji hao ambao ni wananchi wanyonge wa Taifa hili na wanahitaji msaada wa Serikali.

Kamati imeelezwa kua wana jamii hawa mamepatiwa mikopo lakini utaratibu wa kurudisha mikopo hiyo kwao ni chanamoto kwavile wanachokipata kupitia kazi zao hakiakisi marejesho wanayotakiwa kurudisha.

## MAONI, USHAURI NA MAAGIZO YA KAMATI

1. Tunaiomba Serikali kuwafikiria wafugaji wetu hapa nchini kwa kuwaengezea mafunzo na kuwapa mikopo pamoja na kuwaekea utaratibu mzuri wa kufanya marejesho.

2. Kamati inaishauri Wizara ya Biashara kuwasaidia masoko wafugaji wetu ili maziwa wanayoyapata waweze kua na soko la uhakika.

3. Tunaiomba Taasisi yetu ya ZBS kukaa na wafugaji wetu na kuwapatia taaluma ya kuzingatia ubora katika bidhaa zao wanazozalisha.
4. Kamati inaagiza Wizara kuhakikisa kikundi hicho kinalipwa deni lake ambalo wanaidai Serikalini kwa kipindi cha muda mrefu linalotokana na uuzwaji wa maziwa katika kiwanda maziwa cha Bakhresa kilichokuwepo fumba.

## 6.9 HITIMISHO

Katika kutekeleza wajibu wake kwa mujibu wa Katiba ya Zanzibar, Kanuni za Baraza la Wawakilishi na Sheria nyenginezo, Kamati imetoa maelekezo, maagizo na ushauri wake ambao tunaamini kuwa utasaidia katika kuleta ufanisi katika kutekeleza majukumu ya Serikali kupitia Wizara ya Kilimo, Umwagiliaji, Maliasili na Mifugo, Wizara ya Biashara na Maendeleo ya Viwanda na Wizara ya Utalii, Wizara ya Uchumi wa Buluu na Uvuvi, Wizara ya Nchi Afisi ya Rais, Kazi, Uchumi na Uwekezaji na Wizara ya Utalii na Mambo ya Kale. Maoni na Ushauri uliotolewa na Kamati una lenga kuwawakilisha vyema wananchi wa Zanzibar na kuona kuwa maslahi ya wananchi hao, kwa mujibu wa sheria yanapewa kipaumbele. Kamati yetu inatumai kuwa maelekezo na maoni yote yaliyotolewa na Kamati kwa Wizara hizo yatazingatiwa kwa lengo la kutoa huduma zilizo bora zaidi kwa wananchi wote wa Zanzibar. Kamati inatoa shukurani zake za pekee kwa Spika wa Baraza la Wawakilishi, Katibu wa Baraza la Wawakilishi na watendaji wote wa Afisi ya Baraza la Wawakilishi, kwa kuiwezesha Kamati hii kutekeleza majukumu yake vizuri, lakini zaidi kwa ushauri walioupatia Kamati yetu katika kipindi chote cha utekelezaji wa majukumu yake.